UKURASA 20



**Atakayempata mbwa wa Wema kulamba mil. 2**

## Lukuvi amaliza mgogoro sugu wa ardhi baina ya wananchi, kiwanda



UKURASA 3

**MAISHA**

Machi 14, 2021 Nipashe Baba, Mama na Mwana *Jumapili*



**HARUSI**

Ukurasa 12



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Hivi ndivyo wanaume wanavyopenda mazingira nyumbani yawe muda wote

**Furahia kabichi ya mayai**

Ukurasa 14



**MAAJABU YA PARACHICHI**

**Katika kutunza nywele zenye afya**



Jumapili Machi 14, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580519

JUMAPILI

# KIMEWAKA

**KAMATAKAMATA** uzushi aliko JPM yaanza, fundi simu mbaroni, Kigogo wa mitandaoni asakwa...*Endelea uk. 2*



## Watu 600 'wapiga nyungu' Muhimbili

UKURASA 2


UKURASA WA 3

## MKURUGENZI ABAINI SHIDA MTOTO MKALI WA HESABU

MKURUGENZI wa Elimu, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Julius Nestory, ameushauri uongozi wa Mkoa wa Morogoro, kuchukua jukumu la kumwendeleza kimasomo mtoto Charles Mbena badala ya watu binafsi...

## Simulizi za chifu aliyezikwa pamoja na watu wakiwa hai

UKURASA 5



Rais John Magufuli



Picha iliyosanifiwa inayotumiwa na anayejiita Kigogo

**MICHEZO** **MASHABIKI SIMBA WAPIGWA 'STOP'** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Fundi simu mbaroni kisa taarifa za JPM

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi linamshikilia fundi simu, Charles Majura (35), kwa tuhuma za kufanya kosa la kimtandao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Ramadhani Kingai, alithibitisha kushikiliwa kwa mtuhumiwa huyo jana.

Kamanda Kingai alikuwa anazungumza mkoani Pwani baada ya kikao kilichojumuisha makamanda wa polisi wa mikoa minne ya Pwani, Morogoro, Tanga na Kinondoni.

Majura anadaiwa kusambaza taarifa za uzushi kwamba Rais John Magufuli ni mgonjwa.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi wa watu pindi wanapotumiwa taarifa za uzushi, nao wamekuwa wakizisambaza bila kujua kuwa ni kosa kisheria.

"Watu wanaosambaza taarifa za uzushi za uongo kwenye mitandao ya kijamii kwamba Mheshimiwa Rais ni mgonjwa, wanaleta hofu kwa wananchi.

"Taarifa hizi tumeanza kuzifanyia kazi. Machi 11, mwaka huu, tulimkamata Charles Majura ambaye ni kinara wa kusambaza taarifa hizi, ni fundi wa simu," alidai.

Kamanda Kingai alisema wanaendelea kumshikilia mtuhumiwa huyo huku Jeshi la Polisi likikusanya ushahidi kuhakikisha anapelekwa mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.

"Bado tunafuatilia watu wengine ambao wanasambaza taarifa hizi za uzushi, yeyote anayesambaza tutamkamata. Tutahakikisha tunapekua kila sehemu kuhakikisha tunawakamata wote wanaoleta hofu kwa taarifa ambazo ni za uongo.

"Nitoe rai kwa Watanzania wengine ambao hawajui, kutokufahamu sheria siyo kinga ya kushtakiwa, kwamba ukikutana na taarifa ya uzushi kwenye mtandao usisambaze, kusambaza ni kutenda kosa.

"Taarifa hizi za kizushi, tutazifanyia kazi kuhakikisha wote wanaohusika watakamatwa na kushtakiwa kwa mujibu wa sheria," alisema.

**WAMSAKA KIGOGO**

Kiongozi huyo wa polisi pia alisema jeshi hilo linamsaka mtu anayejiita Kigogo, likimtuhumu kutoa taarifa linazoziita za upotoshaji kwenye mitandao ya kijamii.

Alisisitiza kuwa Kigogo ni mhalifu kama wahalifu wengine ambaye wanaendelea kupekua kuhakikisha anatiwa mbaroni.

"Huyu anayeitwa Kigogo ni mhalifu kama wahalifu wengine, Naye tunaendelea kupekua kuhakikisha tunamtia mbaroni kwa muda, siku haijafahamika ila atakamatwa tu," alisisitiza.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Humphrey Polepole (kushoto), akifafanua jambo kwa wajumbe wa kamati hiyo, walipotembelea na kukagua ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Azania, jijini Dar es Salaam jana. Wa tatu kushoto ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, David Silinde. **PICHA: BUNGE**

# 600 wapiga nyungu Muhimbili

**Na Romana Mallya**

WATU 600 wamejitokeza kupiga nyungu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MHN) ndani ya siku 10 tangu kufungwa kwa mashine maalum ya kutoa huduma hiyo kwenye hospitali hiyo ya ngazi ya juu zaidi nchini.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano cha hospitali hiyo, Aminiel Aligaesha, aliliambia Nipashe jana asubuhi, jumla ya watu 600 wamejitokeza kupatiwa huduma hiyo tangu kuzinduliwa rasmi kwa huduma hiyo Machi 4, mwaka huu.

Alisema wanaendelea kuwakaribisha wananchi kwenda katika matawi mawili ya hospitali hiyo yaliyoko Upanga na Mlongazila mkoani Dar es Salaam ambako kumefungwa mashine hizo za kujifukiza.

"Mpaka sasa, wamejifukiza watu 600. Kati yao, Upanga wamejitokeza 550 na Mlongazila 50. Kwa hiyo, wananchi wanaalikwa kuendelea kutumia huduma hii Upanga na Mlongazila," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Prof. Lawrence Museru, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mashine hizo (tatu zimefungwa Upanga na moja Mlongazila), alisema huduma hiyo inatolewa kwa Sh. 5,000 kwa kila mtu.

Hata hivyo, alisema huduma hiyo ni kwa wagonjwa ambao wanaweza kusimama na kutembea wenyewe na wananchi wanaotaka kujifukiza kujikinga na maradhi.

Alisema hospitali imezifunga mashine nne kwa ajili ya kujifukiza na kila moja imenunuliwa kwa Sh. milioni 7.5.

# Tembo wavamia vijijini

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

UONGOZI wa Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa, umeanza operesheni maalum kuyafukuza makundi tisa ya tembo waliovamia vijiji vya Limba na Kafukoka na kuharibu mazao kwenye mashamba ya wakazi wa vijiji hivyo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Carlolius Misungwi, alisema jana kuwa operesheni hiyo imeanza kutokana na tembo hao kula mazao kwenye mashamba ya wakazi wa vijiji hivyo, hali inayosababisha upungufu wa vyakula katika vijiji hivyo.

Alisema kuwa kutokana na tembo hao kuvamia vijiji hivyo, wananchi wamekuwa wakiishi kwa hofu huku muda mwingi wakiwa wamejifungia ndani wakihofia maisha yao kutokana na kuongezeka kwa tembo hao.

"Hali hii ni hatari kwa maisha ya wananchi, lakini pia wanyama hao wamekuwa wakila mazao waliolima wananchi hao kiasi kwamba huenda vijiji hivyo vikakabiliwa na upungufu wa chakula katika mwaka huu," alisema.

Hanry Wiso, Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Kalambo, alisema kuwa tangu mwanzoni mwa mwaka jana, kulianza kuonekana tembo wawili maeneo hayo, lakini wameongezeka hadi kufikia 72 katika makundi tisa na wamekuwa wakiishi katika mapori yaliyopo karibu na vijiji hivyo.

Alisema wamepata bunduki mbili maalumu kwa ajili ya kuwafukuza tembo hao na kuwaelekeza katika msitu wa Mto Kalambo ambao unapita kwenye mapori ya akiba ili wakaishi huko.

Mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Kafukoka, Antonia Mbalamwezi, aliishukuru serikali kwa uamuzi huo kwa kuwa maisha ya wakazi hao yalitawaliwa na hofu kutokana na tembo kuzagaa katika vijiji vyao.

Alisema amani ilikosekana kwa wazazi pindi watoto wao walipokuwa wanakwenda shuleni kwa kuwa walikuwa wakihofia kupoteza maisha kwa kuuawa na tembo hao.

# HABARI KITAIFA



Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Kalobelo (katikati), akizungumza na Ofisa Elimu wa mkoa huo, Mhandisi Mwalimu Joyce Baravuga, aliyembeba mtoto mwenye kipaji maalum cha hesabu, Charles Mathias Mbena, walipomtembelea mtoto huyo, katika tarafa ya Matombo, wilayani Morogoro hivi karibuni. Kushoto ni baba mzazi wa mtoto, Mathias Carol. **PICHA: IDDA MUSHI**

## Lukuvi amaliza mgogoro sugu wa ardhi baina ya wananchi, kiwanda

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amemaliza mgogoro wa muda mrefu baina ya wananchi wa eneo la Chasimba, Chatembo na Chachui katika kata za Bunju na Wazo, Manispaa ya Kinondoni na Kiwanda cha Saruji cha Tanzania Portland.

Katika hitimisho la mgogoro huo, kampuni hiyo inayozalisha saruji aina ya Twiga, imekubali kuachia hekta 224.8 kati ya 922.55 kwa wananchi wa eneo hilo.

Uamuzi wa wananchi kuachiwa hekta 224.8 unatokana na serikali kuingilia kati mgogoro huo mwaka 2015 baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi na kuamua kutafuta suluhu ya kuangalia namna bora ya kutekeleza uamuzi wa Mahakama ya Rufani.

Akizungumza jana na wananchi wa eneo hilo, Lukuvi alisema baada ya mazungumzo marefu na uongozi wa kiwanda ikiwamo bodi ya wakurugenzi, wamiliki wa kiwanda hicho walikubali kuachia eneo lake lenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 60 kwa wananchi.

Waziri Lukuvi alisema mwelekeo wa serikali ni kutetea wanyonge na shukrani kubwa apewe Rais John Magufuli kwa uamuzi wa kuwatetea wananchi hao na kusisitiza kuwa uamuzi wa kutovunja nyumba za wananchi wa maeneo hayo, hauingilii ule wa Mahakama ya Rufani bali unalenga kunufaisha pande zote mbili.

Alisema kutokana na suluhu ya mgogoro huo, sasa kila mwananchi katika eneo hilo atatakiwa kulipa gharama za kumiliki ardhi ambazo ni Sh. 6,400 kwa mita ya mraba ikiwa ni juhudi za serikali wakati wa majadiliano.

Lukuvi alisema awali, wamiliki walitaka wananchi kulipa Sh. 20,000 kwa mita za mraba na kuongeza kuwa kuanzia leo, wananchi hao watapatiwa ankara za malipo kujua kiasi wanachotakiwa kulipa katika eneo hilo lenye mitaa mitatu ya Boko, Basihaya na Wazo.

"Eneo hili mlilovamia ninyi lina mambo mawili. Kwanza wenye eneo wana hati za umiliki pamoja na leseni za madini na ninyi mmezuia kiwanda kufanya kazi. Mimi nilinunua kesi na kufanya jambo hili kwa miaka mitano na nimetumia kila uwezo wangu na leo (jana) nahitimisha suala hili," alisema.

Waziri Lukuvi alimwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Sipora Liana, na timu yake kwenda katika eneo hilo na kukagua maeneo yanayohitajika kwa ajili ya shughuli za huduma za jamii kama vile shule na zahanati ili kuanza ujenzi kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo wanahitaji huduma hizo.

Pia alipiga marufuku wananchi kuanza kuvamia tena maeneo ya kiwanda na kusisitiza kuwa hakutakuwa na huruma ya kuongeza mita za mraba katika eneo hilo kwa watakaovamia.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, alimshukuru Waziri Lukuvi kwa kusimamia na hatimaye kutatua mgogoro huo na kubainisha kuwa kutokana na kazi kubwa inayofanywa na wizara, kwa sasa migogoro ya ardhi kwenye wilaya yake imepungua. Alisema awali Kinondoni ilikuwa ikioongoza kwa migogoro ya ardhi kwa asilimia 75.

Mkazi wa Chasimba, Semeni Charles, aliishukuru serikali kwa kutetea wanyonge katika suala hilo na kueleza kuwa sasa wataishi kwa amani tofauti na awali walipokuwa hawajui hatima yao juu ya suala hilo.

Wananchi wa eneo hilo wapatao 932, mwaka 2008 walifungua kesi Namba 129 katika Mahakama ya Rufani Tanzania kuomba kutambuliwa kama wamiliki halali wa eneo hilo lakini walishindwa shauri hilo na kuamuriwa kubomolewa nyumba zao.

Kutokana na suluhu ya mgogoro huo eneo hilo, vimepatikana viwanja 4000 vya ukubwa na matumizi mbalimbali pamoja na maeneo ya barabara na huduma za jamii na wananchi waliobakishwa katika eneo hilo, sasa watatakiwa kulipa gharama za kumiliki kulingana na ukubwa wa eneo.

Eneo la Chasimba, Chatembo na Chachui katika kata za Bunju na Wazo ambalo lilikuwa maarufu kwa uchimbaji wa chokaa na kokoto, liliingia kwenye mgogoro mwaka 2008 kati ya wananchi wa eneo hilo na Kiwanda cha Saruji cha Wazo.

Mggoro huo ulitokana na wananchi kuvamia eneo hilo na baada ya kufanyika uhakiki ilibainika kuwa hekta 224.8 zilivamiwa.

## Mkurugenzi abaini shida mtoto mkali wa hesabu

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MKURUGENZI wa Elimu, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Julius Nestory, ameushauri uongozi wa Mkoa wa Morogoro, kuchukua jukumu la kumwendeleza kimasomo mtoto Charles Mbena badala ya watu binafsi.

Mtoto huyo (6), mwanafunzi wa chekechea katika shule ya Msingi Nyingwa mkoani Morogoro, amebainika kuwa na kipaji cha ajabu cha hesabu.

Mkurugenzi huyo alitoa rai hiyo baada ya kukutana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Emmanuel Kalobelo, na timu ya wataalamu wa elimu, viongozi wa Wilaya ya Morogoro, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyingwa na baba mzazi wa mtoto huyo.

Alisema waandishi wa habari wametekeleza jukumu lao kwa kumwibua mtoto huyo na kinachopaswa kufanyika kwa sasa ni kusaidia kuendeleza zaidi kipaji hicho.

Nestory alisema mkoa unapaswa kuendelea na taratibu za kumsaidia zaidi mtoto huyo kwa kupata taasisi au mtu binafsi ambaye atakuwa sahihi kumsaidia mtoto huyo kielimu chini ya mikono ya serikali.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Kalobelo, alisema tayari wameweka vigezo 11 kwa wanaotaka kumchukua mtoto huyo na jopo la wataalamu mbalimbali linashughulikia suala hilo.

Alisema wameweka utaratibu huo ili kuepuka kupata mtu binafsi ambaye akiondoka au kushindwa njiani, ataharibu maendeleo ya kitaaluma ya mtoto huyo.

Kalobelo alisema miongoni mwa vigezo hivyo ni taasisi itakayomchukua kuwa tayari kuwajibika kwa mavazi, chakula, ada na masuala ya kiafya awapo shuleni na hata nyumbani na ikibidi kuwe na akaunti maalum ya fedha kwa ajili ya kuendelea kupokea misaada na kumwekea akiba.

Vigezo vingine ni taasisi kuwa tayari kuwasilisha matokeo ya kitaaluma ya mtoto na shule yake kwa uongozi wa mkoa, kuangalia namna ya kusaidia Shule ya Ningwa kwa namna yoyote, mazingira rafiki yanayofikika na kuwa tayari kuwapokea wazazi wa mtoto huyo pamoja na mambo mengine.

Alisema tayari walijitokeza wadau tisa kuonyesha nia ya kumchukua mtoto huyo, ikiwamo Taasisi ya Fountain Gate, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, Hamis Taletale, shule ya kanisa la Full Gospel ya Dar es Salaam, Shule ya La Miriam, Dickson Nyonga, Charles, Dk. Picks, Mohamed Mkombalo na wengine.

Alisema serikali inatarajia kujenga madarasa mapya manane katika Shule ya Msingi Nyingwa alikoibuliwa mtoto huyo baada ya kukamilika kwa ujenzi unaoendelea sasa wa madarasa mawili na ofisi ya walimu.


### NKAYA COMPANY LIMITED

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **KCB BANK**, wadaiwa wafuatao wanatakiwa walipe deni lao lote ndani ya siku kumi na nne (14) kutokea tarehe ya kutoka kwa hili tangazo. Kushindwa kufanya hivyo kutapelekea kuuzwa kwa mali zao walizoziweka kama dhamana.

| JINA LA MDAIWA | MAELEZO KUHUSU DHAMANA | USAJILI WA DHAMANA | TAREHE & MUDA |
|---|---|---|---|
| ST. VIVIAN SCHOOL | NYUMBA ZA KUISHI | KIWANJA NO.531, KITALU "A", CT NO.43580. ILIYOPO ENEO LA USA RIVER KATA YA ARUMERU MKOANI ARUSHA. MALI INAYOMILIKIWA NA CRISPIN MUGARULA. | 27/03/2021 SAA 04:00 ASUBUHI |
| ZILLY BADI MRUMA | NYUMBA YA KUISHI | SHAMBA NAMBA.2608, CT NO.27216, L.O NO. 308478. ILIYOPO ENEO LA MATEVES JIJINI ARUSHA. MALI INAYOMILIKIWA NA ZILLY BADI MRUMA. | 27/03/2021 Saa 04:00 asubuhi |
| KAC SECONDARY SCHOOL AND JAVIRO SAFARIS LTD | SHULE YA SEKONDARI | KIWANJA NAMBA. 100 NA 101, KITALU "G", CT NO.30614, LO NO.309247, ILIYOPO ENEO LA NGORBOB KATA YA ARUMERU MKOANI ARUSHA. MALI INAYUOMILIKIWA NA NDUGU CARVIN THOMAS MAREALLE. | 27/03/2021 SAA 04:00 ASUBUHI |
| ABDUL AZIZ MANYONYI | NYUMBA YA KUISHI | KIWANJA NAMBA.486, KITALU "V", CT NO.50407, ILIYOPO ENEO LA NGOKOLO MANISPAA YA SHINYANGA, PAMOJA NA KIWANJA NAMBA.1342, KITALU "TT", CT NO.26823, ILIYOPOI ENEO LA LUBAGA NDANI YA MANISPA YA SHINYANGA. MALI INAYOMILIKIWA NA NDUGU ABDUL AZIZ MANYONYI. | 2/04/2021 SAA 04:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

- Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada na asilimia 75% atatakiwa kumaliza ndani ya siku saba endapo atashindwa kulipa kwa muda huo uliowekwa ,pesa aliyolipa haitarudishwa na mnada utarudiwa.
- Ukaguzi wa mnada utafanyika siku ya mnada.
- Gharama za kuhamisha mali au kumtoa mtu ndani pamoja na kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe.
- Dhamana itauzwa kama ilivyo.
- Endapo yeyote atajitokeza kuharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake na kulazimika kulipa gharama za mnada.
- Dalali wa mnada ni Nkaya Company Limited ndio wenye mamlaka na maamuzi ya mwisho ya kumtangaza mshindi.

**NKAYA 0753 000 825/ 0626 180 070**

MAKALA MAALUM

# Madhila yanayozikumba shule kongwe

Na Augusta Njoji, MOSHI

## ●Hiki hapa kiini kuboronga kitaaluma
## ●Jafo azitoa vumbi hadi marumaru



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Machame mkoani Kilimanjaro, wakiwa kwenye moja ya madarasa yaliyofanyiwa ukarabati. **PICHA : AUGUSTA NJOJI**

UCHAKAVU wa miundombinu na wizi umetajwa kuwa ni miongoni mwa kero zilizokuwa zikizikabili shule kongwe za wasichana mkoani Kilimanjaro na kuzifanya kuwa na ufaulu usioridhisha.

Hata hivyo, kero hizo sasa zimegeuka historia baada ya serikali kukarabati na kujenga miundombinu katika shule hizo kupitia Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).Nipashe ilitembelea Shule za Sekondari za Wasichana Machame, Ashira na Weruweru na kushuhudia uboreshaji mkubwa wa miundombinu uliofanywa na serikali huku walimu na wanafunzi wakibainisha madhila yaliyokuwa yanawakumbuka awali.

Makamu Mkuu wa Shule ya Wasichana Machame, Evarist Swai, anasema shule hiyo ilianza mwaka 1947 na ilikuwa haifanyiwi ukarabati na hivyo majengo yake kuchakaa.

Anasema kutokana na hali hiyo, mwaka huu wa fedha, serikali imetoa fedha za ukarabati na ujenzi zaidi ya Sh. milioni 900 ili kurudisha hadhi ya shule hiyo.

"Kabla ya ukarabati, hali ya miundombinu ilikuwa mbaya sana, ilikuwa imechoka, madarasa yalikuwa yamechakaa, mabweni yalikuwa ni chakavu kiasi cha kukatisha tamaa watoto wa kike, lakini kwa sasa mtu akija, anafikiri ni chuo kikuu," anasifu.

Mkuu wa Shule ya Wasichana Ashira, Elizabeth Abdallah, anasema shule hiyo ilijengwa mwaka 1961 na majengo yaliyokuwapo awali kabla ya ukarabati, yalikuwa kikwazo kwenye kufundisha na kujifunza.

"Ukarabati huu umeonyesha namna ya kumthamini mtoto wa kike kwenye shule kongwe. Hii shule tumepokea zaidi ya Sh. milioni 800," anasema.

Kiongozi huyo wa shule anabainisha kuwa kwa sasa miundombinu iliyopo inajitosheleza na bweni lililoteketea kwa moto limejengwa na wanafunzi wanalitumia.

Mkuu wa Shule ya Wasichana Weruweru, Rosalia Frimi, anasema shule ilikuwa na uchakavu wa majengo, mfumo wa umeme na majitaka, hali iliyokuwa kero kwa wanafunzi."Hii shule ilianzishwa mwaka 1963. Kabla ya ukarabati uliofanyika, kulikuwa na hali mbaya ya miundombinu. Mabweni yalikuwa yanavuja maji.

"Tumepokea Sh. milioni 749, wanafunzi wamefurahi kutokana na kuwapo kwa mazingira mazuri ya kujifunzia," anasema.

WANAFUNZI WANASEMAJE?

Mwanafunzi wa Weruweru, Raketi Ranti, anasema mabafu yalikuwa mawili tu shuleni kwao, hali iliyowalazimu kutumia muda mrefu na kuoga kwa foleni, hivyo ukarabati na ujenzi uliofanyika umesaidia kuondokana na tatizo hilo.

Akizungumzia kero kwenye maabara, Happiness Kiyawiga, anasema kulikuwa na uchakavu uliosababisha kuingia kwa awamu kujifunza kwa vitendo, lakini sasa miundombinu imetengenezwa na maabara zinavutia.

"Kwenye mabweni, paa lilikuwa linavuja na kulowanisha vitu vyetu, lakini sasa hakuna tatizo, mfumo wa vyoo maji yapo, tunashukuru serikali kwa kuiboresha shule hii," anapongeza.



Mwonekano wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira baada ya kukarabatiwa. **PICHA : AUGUSTA NJOJI**

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Machame, Rukia Sharrif, anasema kero iliyokuwa inawakabili ni wanakijiji wasiohusika na mazingira ya shule, kuingia na kuiba mali za wanafunzi kwenye mabweni.

"Baada ya kukarabati na kuweka mabweni kwenye usalama, tunashukuru serikali kwa kutusaidia, sasa hatuna vikwazo," anabainisha.

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Ashira, Enerestina Msengi, anasema miundombinu haikuwa rafiki kwa wanafunzi na kusababisha kushindwa kujisomea vizuri.

"Kabla ya ukarabati, madarasa hayakuwa rafiki kujisomea kwa sababu ya ubovu uliokuwapo. Baada ya ukarabati madarasa yamekuwa mazuri na wanafunzi kutumia muda mwingi kujisomea," anasema.

Anatoa wito kwa wanafunzi kusoma kwa bidii ili kufikia ndoto zao kwa kuwa kwa sasa hakuna kikwazo cha miundombinu.

Salome Salala wa shule hiyo, anasema serikali imechangia ufaulu wake kutokana na kuboresha miundombinu.

"Nimeona mabadiliko baada ya kuboreshwa kwa miundombinu. Kwa sasa umeme upo wa uhakika na tunatumia muda mwingi kujisomea na kuongeza ufaulu," anasema.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Paulina Mkwama, anaishukuru serikali kwa kukarabati shule kongwe, akibainisha kuwa shule saba kati ya tisa ukarabati wake umekamilika.

"Tunashukuru serikali kwa kukarabati shule kongwe. Kwa sasa tupo kwenye hatua za mwisho kukamilisha Shule ya Sekondari ya Ufundi Moshi na Shule ya Sekondari ya Wavulana Lyamungo," anasema.

Ofisa huyo anasema miundombinu yake awali ilikuwa imechakaa kwa kiwango kikubwa na kusababisha wanafunzi kushindwa kusoma vizuri.

"Kwenye shule hizi za wasichana, miundombinu imekuwa rafiki kwao hasa ikizingatiwa mahitaji yao ya kike, usalama wao umeongezeka baada ya kukarabatiwa kwa miundombinu ya shule," anafafanua.

Kutokana na miundombinu hiyo kuvutia, ofisa huyo anasema baadhi ya wanafunzi, wakati wa likizo wamekuwa wakiomba kubaki shuleni kuendelea kusoma katika mazingira rafiki."Sisi Kilimanjaro tunataka kutokomeza daraja sifuri na la nne kwenye mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne na sita.

"Tunataka kutoa wataalamu wa fani mbalimbali wenye ujuzi wa kweli. Tunataka kuandaa rasilimali watu yenye ujuzi," anatamba.

Anasema hakuna sababu ya kupata madaraja hayo kutokana na jitihada za ufundishaji zinazofanyika sambamba na uboreshaji wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

"Tumeweka lengo ifikapo mwaka 2022, tufikie asilimia 50 ya wanafunzi wa wasomo ya sayansi, na tunasisitiza watoto wa kike kusoma masomo haya," anasema.

Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Moshi, Juma Tukosa, anasema ukarabati wa shule kongwe umefanyika kwenye shule za wavulana ikiwamo ya Ubwe ambayo ilipokea zaidi ya Sh. milioni 900 na ukarabati wake umefanyika vizuri.

HABARI KITAIFA



Kaburi alilozikwa Chifu Mharule Gama pamoja na watu wawili wakiwa hai mwaka 1889.
**PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

# Simulizi za kuvutia Chifu wa Wangoni alivyozikwa na watu wawili wakiwa hai

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MOJA ya vivutio vya utalii wa kiutamaduni vinavyopatikana katika Kijiji cha Mbingamharule, Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma ni uwapo wa kaburi la duara ambalo Chifu Nkosi Mharule bin Zulu Gama, alizikwa mwaka 1889.

Mambo ambayo yanawashangaza wengi wanaotembelea kaburi hilo. Ni historia inayoonesha kuwa Nkosi Mharule baada ya kufariki dunia, alizikwa kwa desturi na mila za kichifu za kabila la Wangoni ambao asili yao ni Afrika Kusini.

Christian Ngonyani, mwenye umri wa miaka 87, mzee wa mila katika Kijiji cha Mbingamharule, anasema kijiji hicho kimepewa jina la chifu huyo ambaye alitokea Afrika Kusini na kutawala Ungoni kuanzia mwaka 1847 hadi 1889 alipofariki dunia na kuzikwa katika kijiji hicho.

"Chifu Mharule baada ya kufariki dunia, alizikwa kwa taratibu za jadi za machifu wa Afrika Kusini. Kaburi lake lilikuwa la mviringo, sanda yake ilikuwa ya ngozi na alikalishwa kwenye kiti cha ngozi. Walikamatwa watu wawili wakiwa hai na kuzikwa naye wakiwa wamesimama mbele na nyuma ya chifu," anasimulia Mzee Ngonyani.

Kwa mujibu wa Mzee Ngonyani, taratibu za kijadi za wakati huo zilitaka mfalme au chifu anapofariki dunia ni lazima azikwe na watu wawili wakiwa hai na kusisitiza kuwa hiyo ilikuwa amri ya serikali ya jadi na hapakuwapo mtu alipinga.

Mzee Ngonyani anasema wengi waliokuwa wanazikwa wakiwa hai na mfalme ni wale ambao walikuwa wamezoeana na kufanya kazi naye kwa karibu.

Hata hivyo, anasema kaburi hilo linatumiwa na wananchi wa kijiji hicho kwenda kuhiji kila mwaka. Kaburi hilo liko kilometa mbili toka kijijini hapo na kwamba ndugu wa Chifu Mharule toka Afrika Kusini huwa wanafika kufanya matambiko mahali hapo.

Mwaka juzi, kwa mfano, ukoo wa Mharule toka Afrika Kusini walifika kushuhudia kusimikwa kwa Chifu Nkosi Imanuel Zulu Gama wa Tano ambaye ndiye chifu wa Wangoni kwa sasa.

Anasema yeyote ambaye anapenda kutembelea kaburi hilo, kuna taratibu zake za kimila zikiwamo kubeba unga wa mhogo, mahindi na ulezi ambao unatengenezwa na bibi katika kijiji hicho.

Baada ya kufika eneo la kaburi, anatangulia mhusika ambaye anawasiliana na chifu kwa lugha ya jadi ndipo wanaoitwa waliofika kutambika na kupiga magoti juu ya kaburi na kuomboleza kwa sala za jadi.

"Baada ya maombi, kuku au mbuzi wanachinjwa juu ya kaburi la Chifu Mharule. Jambo la kushangaza mbuzi anapochinjwa hapigi kelele. Baada ya kuchinja mmoja anamwaga unga wote juu ya kaburi",anasema.

Hata hivyo, anasema baada ya kuchinjwa, mtu akienda asubuhi juu ya kaburi haoni damu wala unga, vyote vinakuwa vimeliwa na kwamba hiyo ndiyo ishara ya kukubaliwa shida zote ambazo mtu alikwenda kuomba kwenye kaburi hilo.

Agnes Ngonyani, Msaidizi wa Mzee Ngonyani anasema wanapokea wageni wengi wanaotembelea kaburi la Chifu Mharule kutoka nchi za Ulaya, Marekani na Afrika ambao wanakwenda kwa shida mbalimbali zikiwamo kuhiji na kufanya matambiko.

"Nimekuwa nawapeleka watu wa kawaida, waganga wa jadi, watalii na wagonjwa wanaenda kufanya maombi kwenye kaburi la Chifu," anasema.

# Bunge labaini madudu Jangwani na Azania

**Na Mary Geofrey**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, imeitaka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuwasilisha taarifa ya ukarabati wa shule kongwe za Jangwani na Azania ndani ya siku 30.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Humphrey Polepole, baada ya kamati kuzuru katika shule hizo na kubaini vikwazo kadhaa ikiwamo uchakavu wa miundombinu licha ya ukarabati uliofanyika.

"Tunakuomba Naibu Waziri wa TAMISEMI (Silinde), utuletee taarifa ya kina kuhusu ukarabati wa miundombinu ya shule hizi kongwe ndani ya siku 30, ili kamati ibaini kwa kina changamoto zilizopo na maeneo ya kuyafanyia kazi," aliagiza.

Naibu Waziri wa TAMISEMI, David Silinde, aliihakikishia kamati hiyo kuwa atawasilisha ripoti ya ukarabati wa shule hizo ndani ya wiki moja.

Kamati hiyo pia ilitembelea na kukagua ujenzi wa Barabara ya Shekilango ambayo ni moja ya utekelezaji wa Mradi wa Kuendeleza Jiji la Dar es Salaam (DMDP) katika Wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke wenye thamani ya Sh. bilioni 660 ambazo ni mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia (WB).

Awali, akiwasilisha taarifa ya mradi huo, Mratibu wa Mradi huo, Humphrey Kanyenye, alisema ujenzi wa Barabara ya Shekilango chini ya DMDP ni miongoni mwa miradi mingine minane inayotekelezwa na Manispaa ya Kinondoni.

Alisema mradi huo umekamilika na umeanza kipindi cha matazamio cha mwaka mmoja hadi Machi mwaka 2022. Alisema gharama za ujenzi wa barabara hiyo na zingine ndogo nne zenye uwezo wa kuhimili hali zote bila kufanyiwa matengenezo kwa miaka 20, unatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 26.186.

Alifafanua kuwa Barabara ya Shekilango yenye urefu wa kilomita 3.65 na njia nne, imejengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.773, Barabara ya Akachube yenye urefu wa kilomita 0.94 kwa gharama ya Sh. bilioni 1.285 na Barabara ya Igesa yenye urefu wa kilomita 0.64 kwa gharama ya Sh. bilioni 1.285.

Zingine ni Barabara ya Mori yenye urefu wa Km 0.93 kwa gharama ya Sh. bilioni 1.934, Barabara ya TRA yenye urefu wa Km 1.09 kwa gharama ya Sh. bilioni 1.247 na ujenzi wa madaraja mawili kwa Sh. milioni 669.

"Gharama hizi zinahusisha pia ujenzi wa maegesho ya magari ya zaidi ya 450 kwa mara moja kando ya barabara kwa kuzingatia kuwa barabara ya Shekilango na TRA zinapitia kwenye maeneo ya kibiashara pamoja na kujenga njia za watembea kwa miguu kwa usalama wao.

"Pia, kuna ujenzi wa mifereji mikubwa ya zege kando ya barabara kwa ajili ya kutiririsha maji ya mvua," alisema Kanyenye.

Alibainisha kuwa kazi inayoendelea kwa sasa, ni kuweka taa 280 za barabarani zinazotumia umeme wa jua ili kuimarisha usalama hasa nyakati za usiku kwa gharama ya Sh. bilioni 1.345.

Alisema ujenzi wa taa za kuongozea magari kwenye makutano ya Barabara ya Shekilango na barabara za Simu 2000, Makanya, Igesa, Mori na TRA unafanyika kwa gharama ya Sh. milioni 737.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, alimshukuru Rais John Magufuli kwa kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ambayo ina lengo la kutatua kero za wananchi, kuongeza nafasi ya ajira kwa Watanzania na upatikanaji wa mapato.

"Mkoa tumeweka nguvu katika usimamizi wa miradi kwa sababu imetolewa fedha nyingi, hivyo tutaisimamia ili ambayo bado ikamilike kwa wakati.

"Japo miradi mingine ina matatizo, lakini hatutarudia kosa na tumejitahidi kurekebisha ili zisijirudie tena," alisema Kunenge.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania tuwe makini matumizi mitandao, simu

**MAENDELEO** ya sayansi na teknolojia yanashika kasi duniani, hali ambayo imesababisha pamoja na mambo mengine, nyenzo za mawasiliano kuongezeka na kuboreshwa kila uchao.

Hali hiyo imesababisha watu kuwasiliana kwa haraka zaidi kuliko ilivyokuwa zamani kwa sababu upashanaji habari umekuwa wa kiwango cha juu tofauti na miaka ya 1990 na kurudi nyuma. Matumizi ya simu za mikononi, intaneti, mitandao ya kijami kama YouTube, Instagram, Facebook na Twitter yameshika hatamu na kufanya mawasiliano kuwa rahisi.

Hatua hiyo pia imesaidia kwa kiasi kikubwa kukua kwa biashara za mtandaoni na hata matumizi mbalimbali ya huduma zikiwamo za afya, elimu na mikutano kwa njia ya video.

Pamoja na manufaa hayo makubwa ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kumekuwa na matumizi mabaya ya mitandao ikiwamo kurusha habari za uzushi, matusi na hata kuchafua watu wengine. Baadhi ya watu wamekuwa wakitumia mitandao hiyo kwa kuwashambulia hata viongozi kuhusu mambo mbalimbali ikiwamo kutumia lugha zisizo za staha dhidi yao.

Katika siku za karibuni, mathalani, mitandao hiyo iliibua taharuki kutokana na baadhi ya watumiaji kuanza kuchokonoa habari za Rais John Magufuli huku wakihoji yuko wapi kutokana na kutokuonekana kwa zaidi ya wiki moja katika matukio ya kiserikali kama ambavyo ilizoeleka.

Baadhi ya watumiaji hao wa mitandao, bila kuuliza wahusika waliopewa ridhaa ya kutoa taarifa za serikali, zikiwamo za Rais na wasaidizi wake wakuu, walidiriki kudai na kusambaza taarifa kwamba kiongozi huyo mkuu wa nchi ni mgonjwa mahututi na yuko nje ya nchi kwa matibabu.

Taarifa hizo kwa jumla, zilisababisha taharuki miongoni mwa Watanzania na kuzidisha uvumi, jambo ambalo ni hatari kwa usalama wa nchi.


Kutokana na kuenezwa kwa taarifa hizo, Jeshi la Polisi limeshaanza operesheni ya kuwasaka wale wote waliobua na kusambaza taarifa hizo na tayari linamshikilia fundi simu mkoani Dar es Salaam kwa tuhuma za kusambaza taarifa za uzushi kwamba Rais ni mgonjwa.

Akitoa taarifa za kukamatwa kwa kijana huyo, Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, Ramadhani Kingai, alisema kusambazwa kwa taarifa hizo kumeibua hofu kwa wananchi huku akibainisha kuwa bado wanawatafuta watu wengine waliohusika na sakata hilo.

Ni vyema Watanzania tukachukua tahadhari juu ya matumizi ya mitandao na njia za mawasiliano kwa kuwa isipotumiwa vyema, inaweza kusababisha matatizo. Tunasema hivyo kwa sababu kuna sheria zinazoongoza matumizi ya mitandao na kuna adhabu zinazoweza kuwakumba wanaokwenda kinyume ikiwamo kufungwa jela.

Kama wahenga wasemavyo sumu haionjwi, vivyo hivyo matumizi hasi ya mitandao ya kijamii na simu za mkononi yanaweza kusababisha madhara, hivyo kila mtu achukue tahadhari. Kinga ni bora kuliko tiba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Vyama vya siasa vikumbuke kuwa mwanzo wa uchaguzi ujao ni sasa

**NI** miezi minne sasa tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka jana, huku CCM ikiibuka na ushindi wa kishindo kuanzia ngazi ya udiwani, ubunge na hadi urais.

Kwa kawaida, kumalizika kwa uchaguzi, huwa ndio mwanzo wa maandalizi ya uchaguzi mwingine, hivyo vyama vya siasa ambavyo vinajiandaa kushiriki katika uchaguzi mkuu wa 2025 havina budi kujiandaa sasa.

Maandalizi hayo ni muhimu yaende sambamba na kuandaa wagombea wa nafasi mbalimbali ili wakati ukifika, vyama visipate shida ya kupata wawakilishi kwenye uchaguzi huo.

Bila kuwaandaa wagombea hawa vijana, vyama vinaweza kujikuta katika wakati mgumu na kusababisha viunge mkono wagombea ambao si wanachama wa vyama vyao.

Katika uchaguzi mkuu uliopita, kulitokea kituko ambacho kilifanywa na Chama Tanzania Labour Party (TLP) ambacho kiundani kinaweza kuwa kimetokana na viongozi wa chama hicho kutojiandaa mapema.

Chama hicho kilimtangaza Dk. John Magufuli wa CCM kuwa mgombea wake wa nafasi ya urais kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

Hali hiyo inaweza kuwa imetokana na chama hicho kushindwa kuandaa wagombea mahiri na kujikuta kikipitisha jina la Dk. Magufuli ambaye si wa chama hicho.

Kutokana na hatua hiyo ya kushindwa kupata mgombea urais, chama hicho kiliamua kuelekeza nguvu kwenye nafasi za udiwani na ubunge, huku urais kikimwachia mgombea wa CCM kwa madai kwamba ndiye anafaa.

Msingi wa sababu za TLP kuchukua uamuzi huo, zilielezwa na Mwenyekiti wake wa Taifa, Augustine Mrema, kuwa ni kukosa mgombea mwenye kiwango cha utendaji kama cha Magufuli!

Kutokana na hali hiyo, chama chake hakikuona sababu za kupoteza muda na fedha kwa ajili ya kuweka mgombea, badala yake kikaunga mkono mgombea wa CCM apeperushe bendera katika uchaguzi huo.

Kwa sababu hizo, ni wazi kwamba, kuna haja kwa vyama vya siasa kuandaa wanachama wake kushika nafasi mbalimbali za uongozi badala ya kuvizia wakati wa uchaguzi ndipo vinaanza 'kuokoteza' wagombea.

Viongozi wa vya siasa hawana budi kutambua kuwa mwisho wa uchaguzi huwa ni mwanzo wa uchaguzi mwingine, hivyo uchaguzi unapomalizika, wanatakiwa kujipanga kwa ajili ya uchaguzi mwingine.

Hatua ya TLP kukaa na kupitisha mgombea wa chama kingine inaonyesha ni jinsi gani chama hicho hakikujipanga vizuri na hakikuandaa wagombea wa kukiwakilisha katika uchaguzi huo.

Uchaguzi mkuu unafanyika kila baada ya miaka mitano, na maandalizi yake yanatakiwa kuanza sasa badala ya kusubiri miezi michache kabla ya uchaguzi ndipo maandalizi yafanyike.

Chama chenye mikakati ya aina hiyo, hakiwezi kufika mbali badala yake kinaweza kujikuta kikikaa na kuunga mkono mgombea wa chama kingine, kwa kushindwa kuandaa wanachama wake.

Bila kuwapo kwa hatua za aina hiyo, vyama vya upinzani vinaweza kuendelea kusindikiza tu badala ya kujipanga na kuwandaa wanachama wake ambao wanaweza kuleta 'kashkash' kwenye siasa za Tanzania.

Wakati mwingine si vibaya kusema kuwa ni udhaifu kwa chama cha miaka mingi kama TLP kushindwa kuandaa wanachama wake kushika uongozi, badala yake kinabaki kuvizia wagombea wa vyama vingine.

Kilichotokea kwa TLP, kinaweza kuwa funzo kwa vyama vingine vya siasa ili kujiandaa na kujitegemea kwa kuwa na wagombea wa kutosha katika nafasi mbalimbali na kuleta changamoto.

Chama kinatakiwa kujivunia wagombea wake hasa kwa jinsi kilivyowaandaa kushika nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama na hata nje, hasa kujiwekea utaratibu wa kung'atuka.

Bahati mbaya karibu vyama vyote vikubwa vya siasa, viongozi wa juu na hasa wenyeviti ni wale wale, ambao wamedumu kwa miaka mingi, kana kwamba hakuna wengine wanaoweza kushika nafasi hiyo.

Viongozi waliopo hawana budi kuandaa viongozi wa kesho watakaoongoza vyama badaye na hata wa kuwania nafasi za udiwani, ubunge na urais katika uchaguzi mkuu pia wakumbuke kuwa ni aibu chama kukosa wagombea.

SAFU

AFYA

# Siri ndani ya mbegu za maboga kwa afya

Na Mwandishi Wetu

MBEGU za maboga ni moja ya viungo vya zamani katika mboga na zimekuwa zikitumika tangu enzi na enzi. Lakini katika miaka ya karibuni, matumizi yake yamekuwa makubwa hasa kutokana na madai kwamba zina manufaa mbalimbali kiafya.

Miongoni mwa manufaa hayo ni kuongeza uwezo wa nguvu za kiume, hivyo kuhimili vilivyo tendo la ndoa. Kutokana na taarifa hizo, watu wamekuwa wakizichangamkia na imekuwa fursa kwa wajasiriamali wanaojishughulisha na uuzaji wa vyakula.

Chakula au kiungo hicho kinaweza kuliwa kikiwa kibichi (kimekaushwa tu), kimekaangwa, kimesagwa au kuchanganywa katika vyakula mbalimbali kama vile keki na mikate.

Utafiti wa kisayansi umebaini mbegu za maboga ni zaidi ya yale yanayoungumzwa na baadhi ya watu juu ya kuimarisha nguvu za kiume. Manufaa kiafya, kwa mujibu wa wanasayansi, ni makubwa yakiwamo udhibiti wa maradhi ya moyo.

Mbegu za maboga zinaweza kutumika zikiwa kama zilivyo au kwa kuchanganya kwenye mboga zikiwa zimeswagwa au kutwangwa na ndivyo zimekuwa zikitumika tangu zamani.

Wanasayansi wanabainisha kuwa mbegu za maboga zina virutubisho muhimu katika kuimarisha afya ya binadamu. Miongoni mwa virutubisho hivyo ni protini, nyuzinyuzi, mafuta, vitamin K, magnesiamu, na madini ya chuma, zinki na shaba ambavyo ni muhimu katika afya na kinga ya mwili.

Mbegu za maboga zinaelezwa kuwa zina vitamini E ambazo husaidia kupambana na sumu mwilini. Kwa mantiki hiyo, ulaji wa mbegu za maboga husaidia mwili kupambana na sumu.

### Kupunguza hatari ya saratani

Viinilishe vilivyomo katika mbegu za maboga vinasaidia kwa kiasi kikubwa kupambana na uwezekano wa mtu kukumbwa na aina mbalimbali za saratani kama ya tumbo, matiti, mapafu, kibofu cha mkojo na utumbo mpana.

Licha ya kuwa na manufaa kiafya katika kupambana na kuzuia hatari ya kupata aina hizo za saratani, mbegu za maboga huimarisha afya ya kibofu cha mkojo na mirija ya uzazi.

"Mbegu za maboga zinaweza kusaidia kupunguza kibofu cha mkojo kutanuka au kuwa kikubwa kupita kiasi au kusababisha tatizo katika njia ya haja ndogo," unabainisha utafiti.

Sambamba na hiyo, mbegu za maboga zina kiasi kikubwa cha madini ya magnesiamu, ambayo hukosekana katika vyakula vinavyoliwa na idadi kubwa ya mataifa ya magharibi. Nchini Marekani kwa mfano, takribani asilimia 79 ya watu wazima wanashauriwa kutumia vyakula vyenye madini hayo kwa ajili ya afya zao.

Kimsingi, madini ya magnesiamu ni muhimu katika kudhibiti shinikizo la damu, kupunguza hatari ya maradhi ya moyo, kutengeneza na kuimarisha afya ya mifupa na kufanya kiwango cha sukari kuwa sawa.



### Afya ya moyo

Mbegu za maboga ni chanzo kikubwa cha virutubisho ambavyo husaidia kudhidibiti sumu mwilini pamoja na madini ya magnesiamu, zinki na 'fatty acids' ambazo husaidia kuufanya moyo katika afya njema.

Utafiti wa kisayansi unaonyesha zaidi kwamba maboga pamoja na mbegu zake vina uwezo wa kuongeza 'nitric oxide' katika mwili ambazo husaidia kuimarika kwa mishipa ya damu na kuimarisha mfumo wa damu katika sehemu mbalimbali za mwili.

### Kushusha sukari

Hii ni habari njema kwa wale wenye tatizo la kisukari. Utafiti unaonyesha kuwa ulaji wa maboga, mbegu za maboga na unga wake pamoja na juisi ya boga vina uwezo mkubwa wa kupunguza kiwango cha sukari mwilini.

Utafiti kadhaa unaonyesha kwamba utumiaji wa juisi ya boga au unga wa mbegu za maboga hupunguza kiwango cha sukari hasa kwa wale wenye aina ya pili (type 2) ya kisukari. Hiyo ni kutokana na kiwango kikubwa cha magnesiamu katika mbegu za maboga ambazo husaidia kuleta matokeo chanya katika ugonjwa wa kisukari.

Majaribio yaliyofanywa na wanasayansi nchini Marekani kwa watu 127,000 waliokuwa na kisukari, ulibaini kwamba vyakula vyenye magnesiamu vilileta matokeo chanya kwa kudhibiti sukari kwa asilimia 33 kwa wanaume na asilimia 34 kwa wanawake.

### Kuongeza mbegu za kiume

Kuchangamkiwa kwa matumizi ya mbegu za maboga kwa ajili ya kuimarisha nguvu za kiume huenda kuna ukweli ndani yake! Hii ni baada ya kubainika kuwa mbegu hizo au unga wake ukiwekwa katika mboga husaidia kuongeza mbegu za kiume (manii).

Hiyo ni kutokana na kuwamo madini ya zinki kwa wingi katika mbegu za maboga. Kiwango kidogo cha madini ya zinki mwilini huhusishwa na kupungua au kiwango hafifu cha mbegu za kiume na tatizo la uzazi kwa wanaume.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania wenzangu nani katuroga?



Na Joseph Kulangwa

**Ni ngumu kuamini, nini kilimsukuma Meya Raibu kutoa agizo hilo na hata alipoulizwa, akazidi kusisitiza kuwa hataki kuona katika 'kikao chake' mtu amevalia barakoa, akiamini kwamba Moshi haina maambukizi, bila hata kutoa ushahidi wa vipimo alivyofanya.**

FIKIRIA unapewa mwaliko, kuwa kesho utakuwa mmoja wa watu watakaotembelea zizi la wanyamapori wilayani kwenu, ambalo hujawahi kulitembelea na kushuhudia wanyama waliomo.

Lakini katika mwaliko huo unahadharishwa, kuwa miongoni mwa wanyama waliopo, ni nyoka ambaye wakati mwingine hutema mate yanayoweza kukuathiri endapo yatakupata hususan machoni.

Hivyo unaambiwa ikiwezekana uvae miwani au kitu chochote kinachoweza kuzuia macho yako, dhidi ya mate ya mnyama huyo hatari. Hivyo unajiandaa huku ukiwa na mshawasha wa kesho kujionea wanyama.

Unatafuta miwani mipana kama ya wachomelea vyuma na kesho hiyo asubuhi unaanza safari ya kuelekea zizini, unawasili na kukuta umati wa watu baadhi yao wakiwa na miwani na wengine bila.

Mwenyeji wenu ambaye anaonekana ndiye msimamizi wa zizi lile, anakushangaeni wenye miwani na kutoa amri ya vueni miwani hiyo, kwa kuwa tu yeye hana, huku akibeza kuwa mate ya nyoka huyo hayana athari kama inavyodaiwa. Unashangaa, lakini kwa kuwa uko ugenini, unavua na kujipa moyo wa liwalo na liwe.

Hata hivyo, unapunguziwa kujiamini, ukiwaza kuona wanyama lakini pia ukijihadhari usipite karibu na nyoka mdaiwa, hivyo badala ya kufurahia ziara sasa unakuwa mwenye wasiwasi huku ukiomba imalizike mapema.

Naifananisha hii na alichokifanya hivi karibuni Meya wa Manispaa ya Moshi, Juma Raibu kwa baadhi ya wajumbe waliovalia barakoa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani kujikinga na Uviko-19, alipowataka kuzivua, akidai Moshi hakuna korona.

Tena akawashangaa kwa nini wao wavae barakoa wakati yeye hakuvaa, kwani kufanya hivyo ni kuwatia wananchi mtafaruku, wa kuwa kuna korona huku hakuna ugonjwa huo, na kutiana hofu isiyo ya lazima. Naamini wajumbe wa Baraza lile walimshangaa bosi wao, kwa hatua yake hiyo ambayo haikutarajiwa.

Walimshangaa kwa sababu watakuwa walijiuliza alitumia kanuni gani chini ya dhamana aliyonayo, kuwalazimisha wananchi kuvua barakoa, huku akijua hata Rais Dk John Magufuli siku chache tu kabla, alitangaza kuwa kuna watu wametuingizia magonjwa ya ajabu.

Ni ngumu kuamini, nini kilimsukuma Meya Raibu kutoa agizo hilo na hata alipoulizwa, akazidi kusisitiza kuwa hataki kuona katika 'kikao chake' mtu amevalia barakoa, akiamini kwamba Moshi haina maambukizi, bila hata kutoa ushahidi wa vipimo alivyofanya.

Watanzania ni watu rahimu sana, wasiotaka makuu, ambapo mtu anaweza kutumia nafasi aliyopewa na umma, kuchezea maisha yao hata kama anayahatarisha, kwani kwao huwa rahisi sana kumwachia Mungu.

Hivi Meya Raibu alikuwa na uhakika gani kwamba hao wananchi waliokwa wamevalia barakoa hawakuwa na maambukizi? Je, kama walikuwa nayo, na kwa kuzingatia mkusanyiko ule na kuvuliwa kule, kimetokea nini kwa waliokaa jirani nao?

Ni nini kilimwaminisha Meya Raibu kuwa Moshi hakuna maambukizi? Anajuaje mwingiliano uliyopo kati ya nchi jirani na Tanzania ambayo inapakana na Moshi? Ipo haja kwa Watanzania kubadilika na kuacha kuwakubalia viongozi kila wanachoamuru hata kama ni kinyume na uhalisia wa mambo.

Hizi amri zinazotolewa mara kwa mara na viongozi zikiwamo za kucharazwa viboko, sasa tuzikatae, kwa kuwa si tu zinaingilia faragha, lakini pia zinakiuka haki za binadamu.

Inashangaza, Rais Magufuli tangu Uviko-19 iingie nchini mwaka jana, hakupata hata siku moja, kukataza watu kuvaa barakoa kokote, ila alikuwa akionesha kufurahi alipoona watu hawakuvaa barakoa kuonesha kuwa tatizo halikuwa kubwa kiasi hicho.

Lakini si amri za, "kabla ya kufunga kikao chetu, niwaombe wote waliovaa barakoa wasimame. Vueni barakoa zenu, manispaa yetu iko salama, mimi mstahiki meya sijavaa barakoa, wewe uliyevaa ina maana unajipenda zaidi!"

Kauli hii inamaanisha meya anadiriki kuweka maisha ya wananchi mikononi mwake! Kwamba kwa kuwa yeye kiongozi hajali, basi na wananchi ambao anawaita 'wangu' nao wasijali! Hii ni sawa na kuwafuga. Akifa yeye nao wafe, kwa kuwa kwao yeye ni kila kitu! Uongozi ni dhamana. Mzee wangu na rafiki yangu George Mkuchika, kazi unayo katika utawala bora. **Alamsiki!**

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Mahindi ya Tanzania kupigwa marufuku Kenya vita ya uchumi



Na Thobias Mwanakatwe

**Mwaka juzi, madereva wa Tanzania wa utalii pamoja na kuwa walifuata taratibu zote walinyimwa kuchukua watalii waliokuwa wanakuja Tanzania kutalii ambao walishukia Kenya.**

WATAALAMU wa mambo ya uchumi wanasema, uchumi ni sayansi ya kijamii ambayo hutafiti uzalishaji, usambazaji na matumizi ya bidhaa na huduma.

Wiki hii kulijitokeza jambo kubwa ambalo limezua taharuki kwa wafanyabiashara na Watanzania kwa ujumla. Hiyo ni baada ya nchi jirani kutangaza kuzuia mahindi kutoka Tanzania kuingizwa katika nchi yao kwa madai yana sumu inayosababisha saratani.

Kibaya zaidi majirani zetu hawa wa muda mrefu sana wametangaza jambo hilo hadharani na wameitangazia dunia hali ambayo kwa mtazamo wangu ni vita ya uchumi au siasa ya uchumi.

Kimsingi vita ya uchumi ipo hata katika nchi zilizoendelea, kwa hiyo Tanzania kuingia katika vita hii, halitakuwa jambo geni bali kinachotakiwa ni kwa serikali kujipanga kuona namna ya kukabiliana nayo.

Kutokana na umahiri wa serikali yetu chini ya Rais John Magufuli, hakuna shaka kuwa vita hii itakuwa nyepesi kuishinda na Mungu atatusimamia na kutuongoza katika kuishinda.

Mfano wa kwamba vita ya uchumi imeanza muda mrefu ni pale mwaka 1776, Jasusi wa Kimarekani William Carmichael alitumwa na taifa lake kwenda kutafiti na kujua ni kwa namna gani nchi hiyo inaweza kuteka soko la tumbaku duniani ambalo lilikuwa limeshikiliwa na Bara la Ulaya. Kipindi hicho Ukraine ilikuwa ikizalisha tumbaku bora kabisa na nyingi duniani.

Jasusi huyo alitokea kwenye kitengo cha intelejensia ya uchumi ambacho hutafiti, kuchunguza mataifa mengine kuhusu uchumi wao na namna ya kuudidimiza. Marekani kwa sasa ni taifa ambalo linachunguzwa sana na China na Korea Kaskazini. Lengo ni kuwadhibiti wasiliteke soko la dunia kwa bidhaa zao au wasiibuke kama 'super power' duniani.

Kwa Afrika Mashariki, Kenya ni taifa ambalo limewekeza kwenye intelijensia ya uchumi na taifa tishio kwao ni Tanzania. Tukumbuke Tanzania ina rasilimali nyingi kuliko Kenya, inanufaika na nafasi yake ya kijiographia na pia haina ukame sana.

Kenya wanajua wazi kuwa isingelikuwa bandari ya Dar es Salaam na Tanga wao wangenufaika sana kupitia bandari ya Mombasa. Bandari zetu zinapunguza sana bidhaa za mataifa mengine kupitia Kenya hili kwao ni tishio. Kenya wanajua kabisa kama sio vivutio vyetu tulivyo navyo basi wao wangeongoza kwa utalii Afrika Mashariki na wangepata pesa nyingi kwenye sekta hiyo.

Mwaka juzi, madereva wa Tanzania wa utalii pamoja na kuwa walifuata taratibu zote walinyimwa kuchukua watalii waliokuwa wanakuja Tanzania kutalii ambao walishukia Kenya.

Tanzania ilivumilia kwa muda lakini ilifika mahali ikajibu kwa kupunguza safari za Shirika la Ndege la Kenya (Kenya Airways) kuja nchini. Walipoona hivyo, wakaondoa lile zuio la madereva wetu wa utalii kuingia Kenya ndiyo maana nchi iliwekeza kwenye kununua ndege kwa kuwa ili ujitawale vizuri lazima uwe na uwezo wa kushindana angani, ardhini na majini.

Mwaka 2018 tuliingia nao tena mzozo wa kiuchumi tukigombea bomba la mafuta toka Uganda lipitie wapi. Wakenya walipiga 'trip' Sana kwenda Uganda kwa Mzee Museveni hatimaye tukawashinda tena kwenye vita ile.

Mwaka jana wakati wa corona, madereva wote wa Tanzania walikuwa hawaruhusiwi kuingia Kenya lakini wa Kenya walikuwa wakiruhusiwa hadi tulipifunga mipaka ya Hororo kule Tanga na Namanga, Arusha, ndipo walitia akili wakatuachia.

Katika suala la mahindi yetu kupigwa marufuku kuuzwa Kenya, nchi hiyo kimsingi haijatutendea haki kama jirani mwema. Tuyapime kama kweli yana sumu.

Tafsiri rahisi ni kwamba mahindi yetu yatakuwa yamekosa soko kwenye nchi zote kwa kuwa tu Kenya imetangaza moja kwa moja kuwa yana sumu.

Kuna maswali mengi ya kujiuliza katika jambo hili, kwamba inawezekana Kenya imeyapata mahindi kwenye mataifa mengine kwa bei rahisi zaidi kuliko hapa kwetu, hivyo wametunyima soko la mahindi kipindi ambacho wana uhitaji mkubwa sana wa bidhaa hiyo kutokana na nzige na corona.

Tulitamka hadharani kuwa wakati watu wakiwa lockdown sisi tulime mahindi tutakuja kuwauzia. Hakika tujipange tuishinde vita hii ya kiuchumi.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI AFRIKA**

## DARASA LA NDOA

# Namna ya kutawala msongo wa mawazo



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

TUNAISHI katika ulimwengu wenye baraka na changamoto nyingi. Changamoto mbalimbali za maisha, kwa sehemu kubwa, ni kisababishi cha msongo wa mawazo.

Kuwa na msongo wa mawazo ni hali ya kawaida na isiyoepukika katika maisha ya binadamu ya kila siku. Pamoja na madhara makubwa ya msongo wa mawazo, jambo hilo (msongo wa mawazo) linaweza kutusaidia kubadili mitazamo yetu, mienendo na namna yetu ya kufanya mambo.

Msongo wa Mawazo ni nini?

Ni hali ya kusongwa na mawazo inayotokana na hali za maisha ya kila siku. Msongo wa mawazo unaathiri mwenendo na hisia za mtu nyumbani kwake, kazini na katika jamii kwa ujumla.

Athari zinaweza kuwa za muda mfupi au muda mrefu kutegemeana na kiwango cha msongo wa mawazo na pale unapodumu kwa muda mrefu. Kwa hiyo, mada hii ni muhimu sana kwani inagusa maisha yetu ya kila siku.

Katika mada hii, tutajifunza mambo matatu ambavyo ni visababishi vya msongo wa mawazo, matokeo ya msongo wa mawazo na namna ya kukabiliana na msongo wa mawazo.

**Visababishi**

Mambo yanayosababisha msongo wa mawazo ni pamoja na pale mtu anapofanya mambo yasiyolingana na hali na uwezo wake alio nao. Mfano ni kujilinganisha na wengine. Hii ni sawa na mtu kuthubutu kujikuna mbali zaidi ya kimo cha mkono wake. Matokeo yake mtu anapata hofu na kupoteza matumaini ya maisha. Sababu zingine ni kutojiamini na kutoridhika; mabadiliko makubwa ya maisha; majanga; kukosa maisha yenye mpango na mwelekeo; hali duni ya maisha; kukosa ajira na mahitaji mengine ya maisha.

Nyingine ni kutokufanikiwa au kutokutimiza malengo yaliyokusudiwa. Kwa sababu ya kukiri kuwa haiwezekani, watu wengi hukata tamaa na hufikia hatua ya kutokuona thamani ya maisha yao tena.

Kufanya kazi nyingi kwa wakati mmoja au kuwa na mambo mengi ya kufanya, wakati mwingine ni chanzo cha msongo wa mawazo. Muda mwingi mtu anafikiria namna ya kufanikisha au kufikia malengo ya kazi hizo. Kutokana na hali hiyo, mtu anajikuta anakabiliwa na shughuli nyingi sana. Mazingira ya namna hii, yamefanya watu wengine hata kusahau muda wa kula na kupumzika. Jambo ambalo ni hatari sana kiafya.

Jambo jingine linalosababisha msongo wa mawazo ni mizigo (machungu) nafsini mwa mtu. Ipo mizigo ya aina nyingi. Mizigo mingine watu wanaitafuta na kujitwisha kwa kujua au kutokujua. Mizigo mingine mtu anatafutiwa na kutwishwa na watu wengine.

Anaweza akakutwisha mumeo, mkeo, mchumba, watoto/mtoto, mzazi, mlezi, jirani, rafiki, mwajiri, mwajiriwa wako, mwalimu, mwanafunzi au mpambe. Nafsi ya mtu inajeruhiwa na kujeruhika. Na kwa kweli, watu wengi wana matatizo ya nafsi zaidi kuliko matatizo mengine ya kiafya.

Tatizo linakuwa kubwa pale mtu anapokosa msaada hasa wa kusikilizwa na kukosa ushauri nasaha. Mtu mwenye msongo wa mawazo anapokosa mtu wa kumjali au kumsikiliza, anakuwa katika hali ya upweke na kuhisi kuwa anapuuzwa, anabezwa, hana thamani na hapendwi.

Hali hiyo inamfanya kuwa mtu mwingine ingawaje ni mtu yule yule. Mtu wa jinsi hii ni rahisi sana kupoteza utu wake. Mtu anakuwa mkatili, anakosa upendo, mjeuri, na kuchukia wengine bila sababu.

Migogoro na tofauti za kimawazo juu ya jambo au mambo fulani ya msingi; na mazingira duni ya kazi pia ni vyanzo vingine vya msongo wa mawazo miongoni mwa watu. Kwa ujumla, changamoto za kimaisha, kikazi na uhusiano mbaya baina ya watu vimekuwa chanzo kikuu cha msongo wa mawazo katika jamii nyingi za Ki-Afrika.

Madhara ya Msongo wa Mawazo

Madhara yatokanayo na msongo wa mawazo yanaweza kuwa makubwa kama mtu anadumu na msongo wa mawazo wa muda mrefu. Ni hakika kwamba, matatizo ya mtu yasipopata ufumbuzi wa mapema humletea mtu madhara ya kimwili, kiroho na kisaikolojia.

Moja ya sababu kuu za watu kuugua magonjwa ya moyo kama vile shinikizo la damu la juu (HBP); ugonjwa wa kisukari; ugonjwa wa kupooza; saratani; kuumwa tumbo na kuanza kuharisha au kutokwa damu bila kuumwa chochote.

Hiyo ni kwa sababu ya kuchoshwa na kuelemewa na maisha ya kila siku. Hali hii inaweza kumtokea mtu kwa wazi au kwa siri. Lakini matokeo yake yanajidhihirisha katika mfumo wa maisha ya mtu. Akili, mwili na roho vinajitambulisha kuwa kuna tatizo. Watu wengine wanajikuta wakijisemesha wenyewe; wanapoteza kumbukumbu, kusahau vitu/mambo; kupoteza uwezo wa kufikiri vizuri, hivyo, kufanya uamuzi usiyo na tija; kukosa usingizi; kupata kizunguzungu; kupata vidonda vya tumbo; maumivu ya mara kwa mara ya mgongo kupata matatizo ya misuli; hasira za mara kwa mara; kufokafoka mara kwa mara au kutukana; kujikinai; kudorora kwa afya ya mwili; kuathirika kwa ngozi ya mwili; kupotea kwa haiba nzuri ya mtu na kupoteza mvuto.

Madhara mengine yatokanayo na msongo wa mawazo ni pamoja na kuumwa kichwa kusikoisha bila kuugua; kukosa hamu ya kula -hata kama chakula kipo na ni kizuri. Lakini kwa baadhi ya watu, msongo wa mawazo unaweza kusababisha hali ya kula kupindukia.

Kwa wanandoa (wanaume na wanawake), msongo wa mawazo unaweza kusababisha wanandoa kukosa hamu na nguvu za kuhusiana kimapenzi. Ushahidi wa kuwapo kwa changamoto hii katika maisha ya wanandoa inaonekana katika matangazo ya biashara hasa ya dawa yanayoonekana kila kunapokucha katika mabango, magazeti na kuwapo kwa wauzaji wasio haba wa dawa zinazodaiwa kuongeza nguvu za kiume na zile za kuwavuta wapenzi.

Baadhi ya watu wamejikuta wakijiingiza katika mambo yasiyoleta tija au hatarishi kama vile ulevi uliopindukia; umalaya; na matumizi ya dawa za kulevya. Wengine wamediriki kuchukua uamuzi ya kujiua au kuua wengine. Msongo wa mawazo ukidumu kwa muda mrefu huweza kusababisha magonjwa ya akili; sonona hata kifo pia.

Zaidi sana, msongo wa mawazo hupunguza ufanisi wa utendaji kazi wa mtu. Utendaji wa kazi haundi inavyotakiwa. Ruhusa kazini huongezeka na kusababisha mtu kutokuwepo kazini mara kwa mara (Absenteeism). Hivyo, uchumi nao unapungua na kudorora.

**●Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.**

# MAISHA

Machi 14, 2021
Nipashe


Baba, Mama na Mwana

Jumapili




## HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Hivi ndivyo wanaume wanavyopenda mazingira nyumbani yawe muda wote

## Furahia kabichi ya mayai

Ukurasa 14



# MAAJABU YA PARACHICHI

## Katika kutunza nywele zenye afya



Ukurasa 14

# Ni mtoto wako lakini unazijua tabiza zake?

**Na Moses Ismail**

NI mtoto wako haswa! Hana mzazi mwingine zaidi ya wewe na mama yake au wewe na baba yake. Ni mtoto wenu na hilo halina shaka kabisa!
Tangu azaliwe mpaka anafikisha umri wa miaka tisa sasa, mmemlea nyinyi wenyewe, hajawahi kulelewa na watu wengine, iwe bibi na babu yake au shangaza na mjomba. Hajawahi kulelewa kabisa na watu wengine.
Kwa umri alionao unaamini kwamba unamfahamu sana, unaamini unajua anachokipenda na asichokipenda na hata wakati mwingine wakati wa 'stori' na marafiki zako pale mnapo ongelea watoto wenu, unazungumzia tabia zake.
Lakini ukweli wa mambo ni kuwa tabia hizo unazozungumzia mbele ya wenzako, juu ya mwanao, si tabia zake halisi za sasa, mwanao hayupo hivyo kabisa. Humjui wala hujui lolote lile kuhusu tabia zake halisi.
Tabia hizo unazozungumzia leo, ni tabia zake za miaka minne mitano iliyopita, wakati ule ulipokuwa na nafasi ya kuwa naye na kuzungumza naye mawili matatu kama baba na mtoto na pia kupima uwezo wa ufahamu wake.
Tabia zake chache za sasa unazo zingumzia, ni zile tu unazoziona mara moja moja unapopata nafasi ya kukaa naye sebuleni na pengine kwa usumbufu anaokupa kwa kutaka kitu hiki na kile.
Kwa mfano, unajua anapenda kucheza mpira kwa sababu kila wakati anakuomba umnunulie vifaa vya mpira kama viatu na jezi ama unajua pia kuwa anapenda kuchora kwa sababu hiyo hiyo, ya kutaka umnunulie vifaa.
Ni kweli kabisa, mtoto wako anapenda kucheza mpira na anapenda pia uchoraji na uko sahihi kabisa kwa kusema hivyo. Ila, unajua ni nafasi gani anacheza kwenye mchezo huo na ana uwezo gani wa uchoraji?
Umeshawahi kuona michoro yake au umeshawahi kushiriki katika mechi moja ya mpira wa miguu anayocheza na kumtia moyo au kumshauri ili afikie mafanikio makubwa zaidi katika mmoja ya jambo hilo analopenda?
Ukweli ni kuwa hujawahi kufanya hivyo hata siku moja kwa sababu nafasi yako ya kufuatilia mambo yake ya kitoto ni ndogo sana na wala huoni umuhimu wa kufanya hivyo. Utapata wapi muda huo?
Mpira na uchoraji ni mifano tu, ila kiuhalisia watoto wana tabia nyingi ambazo pamoja na wazazi kujifanya kuwa wanazijua, ukweli ni kuwa hawazijui kama inavyopaswa kuzijua. Hawana muda wa kukaa nao.
Utazijua vipi tabia za mwanao, ambazo ndizo taswira halisi inayomuonyesha yeye ni nani, wakati huna muda kukaa naye na kuongea naye kirafiki kwa kisizingio cha kukosa muda?
Kupotoka au kutengamaa kwa tabia za mtoto kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na wazazi kukosa kuwapa watoto muda wa kushiriki kwenye

## NA HAMIS KIDAGO

0657 207168

# QUIZ

### LE QUIZ DU WEEK

Weka maneno yafuatayo katika mtiririko utakaoyafanya yalete maana kamili.
Mfano: marguerite/est/La/fleur/une →La marguerite estune fleur.

oiseau/Le/un/est/perroquet
..................................................................

plantesfragiles/Les/rosiers/des/sont
..................................................................

un/saumon/poisson//est/Le
..................................................................

est/erable/arbre/un/L'
..................................................................

citron/est/Le/fruit/un
..................................................................

poireau/un/est/Le/legume
..................................................................

des/Le chien et le chat/animauxdomestiques/sont
..................................................................

bambou/une/Le/est/herbe
..................................................................

qui/méne au success/est/Le/un/pont/fragile
..................................................................

c'est/l'histoire/qui commence/Entre/au depart/nous
..................................................................

d'avoir/Sois/raison/et puis/sûr/vas-y
..................................................................

la durée/le soleil/de la nuit/apparaîtra/Quelquesoit
..................................................................

Jibu kama kwenye huo mfano hapo chini.
Mfano: Tu as une valise? – Oui, j'aiune valise de mon frère.

Vousavez des chaussures de marche? – Oui, j'ai.......chaussures de monpère.

Tu as un appareil photo? – Oui, j'ai.......... appareil photo de moncopain.

Vousavezunetente de camping? – Oui, j'ai............tente de mon cousin.

Tu as unevoiture? Oui, j'ai........voiture de mes parents.

Tu as des skis? – Oui, j'ai.......skis de ma sœur.

Vousavezun sac à dos? Oui, j'ai........sac à dos de ma tante.

Tu as unstylo? Oui, j'ai.........stylo de monvoisin.

Vousavezuneboisson à consommer? Oui, j'ai.......boisson de ma petite amie.

Tu as des lunettes? Oui, j'ai.........lunettes de monami.

Les articles partitifs
Angalia kwa makini mfano huu wa "articles partitifs" katika maelezo yafuatayo, kisha ujibu maswali yatakayofuata kuhusu hizo "articles partitifs".
N.B. (ms) nimasculinsingulier, (fs) nifémininsingulier.
.Cestgentil à toi de faire les courses: alors, s'ilteplaît, tuachetesdu riz (ms), del'eau (fs), de laviande (fs) et de l'huile (fs) et tuprendsde l'argent (ms) dansmon sac.

Malizia maneno yafuatayo kwa kutumia "articles partitifs" zinazoendana.

Du poivre (ms)

.........jambon (ms)

.........huile (fs)

..........parfum (ms)

...........fromage (ms)

...........crème fraîche (fs)

...........pâté (ms)


..........bière (fs)

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO



Zao la mtama linahimili hali gani ya hewa?

MAMA mwenye nyumba alitaka kupandisha kodi, lakini kutokana na ubabe wa wapangaji wake alitafuta mbinu ya kuwaambia.
Mama: Wanangu leo nataka nizungumze na nyinyi
Mpangaji: Kuna nini tena?.. Tuambie tu
Mama: Askari walinifuata wakaniambia humu ndani kuna majambazi, hivyo nataka kubomoa nyumba yangu
Mpangaji: Sisi sio majambazi, ila huko kubomoa nyumba sisi tutakwenda wapi?
Mama: Kila mtu aende alipotoka, labda kwa kuwahurumia nawapa muda wa mwaka mmoja lakini kodi inapanda hadi 40,000
Mpangaji: Tulikuwa tunakuangalia tu, tayari mwanao katuambia kila kitu.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Je, unakijua kile unachokimbilia?

KARIBU tena msomaji wangu tuwe pamoja katika mwendelezo wa makala za safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo hebu tujadili wale watu wanaokuwapo mahali fulani lakini hawajui kwa nini wapo pale. Wanajiona wapo sawa kumbe sivyo. Na hata wakijua, hawawezi kujinasua.

Leo nikupe siri. Ukiona mtu anakimbia, kuna vitu viwili vinamsukuma akimbie. Aidha hicho kitu kipo mbele au nyuma yake. Ukimuona mtu barabarani anakimbia, ama kuna kitu anakiwahi huko mbele au kipo kitu nyuma kimemfanya akimbie. Kwa hiyo kuna nguvu mbili hapa duniani, ile inayomfanya mtu atoke pale alipo. Hii inaitwa 'Msukumo'. Inamsukuma atoke eneo alipo.

Lakini ipo nguvu ya mbele inaitwa nguvu ya 'Mvuto'. Hii inamvuta mtu akimbie. Kwa mfano, kuna foleni, nawe umo ndani ya daladala unataka kuwahi na muda unakwenda. Utakachofanya ni kuteremka kwenye basi na kuanza kukimbia kwa miguu. Kuna nguvu inayokuvuta ukimbilie kule uendako.

Yupo mtu mwingine anakimbia, kumbe kule nyuma kuna jambazi au kibaka.Hapo kuna nguvu iliyoko nyuma inamfanya akimbie. Mwingine ana kodi ya nyumba hajamaliza wakati pia ada za watoto zinamsubiri mbele. Ni nguvu mbili zinazompagawisha mtu katika maisha.

Simba mwenye njaa hupambana kupata chakula. Njaa ni nguvu ya msukumo. Anatoka tu anamwuona swala. Huyu swala ni nguvu ya mvuto.

Huku nyuma njaa inamsukuma, lakini mbele yake kuna nyama. Hii ni nguvu inayoweza kumfanya mtu akimbie kwa kasi au taratibu.

Mpenzi msomaji, ukitaka kujua mbio za mtu, itokee ajali au tukio baya. Hata kama mwili ni mzito, utakuwa mwepesi ajabu. Kasi ya mtu hudhihirika kutokana na kile kilichotokea. Hiyo ni nguvu ya msukuko au mvuto. Na nguvu hizi zipo nzuri na mbaya.

Kijana mmoja nilikuwa namshauri kuhusu hali aliyokuwa akipitia kimaisha akasema; "Siku moja nilikuwa nikipita barabarani nikasikia sauti ikiniambia kaanguke barabarani gari likukanyage".

Akaendelea kusema kuwa siku nyingine akatokewa na hali ya ajabu akawa anatamani kufa. Akatoka akaenda kuketi katikati ya barabara ya treni. Akaiona treni inakuja na ilipomkaribia akili ikamwambia kimbia toka hapo. Akatii akaepuka kifo.

Ni dhahiri kwamba kuna nguvu ya msukumo mbaya iliyompeleka pale. Je, unajua unachokikimbilia? Zipo nguvu za dhambi, zipo tamaa za mwili zinazoangamiza wanadamu. Yapo mambo mabaya yaweza kuwa ni nguvu ya msukumo. Haijalishi ni mbaya au ni nzuri. Cha msingi ni kujiuliza kule unakokimbilia ni wapi?

Wapo watu wanaacha kutafuta nguvu za Mungu wanakimbilia kwa waganga wa kienyeji eti kupata uponyaji au utajiri. Huyo mganga anayekudanganya atakupa pete ya utajiri, mwenyewe anaishi kibanda cha nyasi kilichojaa vibuyu na matunguri. Kwa nini yeye asiwe tajiri? Huu ni mvuto mbaya.

Nguvu ya mvuto iliyoko mbele yako ni ipi? Unatoka spidi, unaenda wapi? Yamkini wanandoa wengi wamejikuta kukwama kwa sababu ule mvuto walioona mara ya kwanza wakati wa uchumba siyo matarajio ya pale walipo hivi sasa.

Ni kweli binti hajaolewa, anakutana na kijana mtanashati kwenye sehemu za starehe. Wanapendana na katika muda mfupi wanatangaza uchumba. Hajui tabia zake wala hajafahamu vema historia ya wazazi au ukoo wake, anakubali ndoa ya haraka haraka.

Hii ni nguvu ya msukumo ikikolezwa na mvuto iliyomtawala binti na kuchukua uamuzi mgumu. Ndoa za aina hii mara nyingi ama zimeishia njiani au zikiendelea zinakuwa na mizozo isiyoisha. Wapo waliojitosa na kugundua kumbe yule alikuwa ni teja.

Vijana badala ya kumshirikisha Mungu awape mwenza sahihi, tamaa zinawavuta. Hata mwanadamu wa kwanza, Adamu, Mungu alimpatia mke aliyemfanyiza toka ubavu wa Adamu. Mungu anaweza yote, wewe mshirikishe utaona miujiza yake kwako.

Ipo nguvu ya matumaini ambayo Mungu ameweka mbele yetu kama ilivyoandikwa, Waebrania 6:18 "ili kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo, Mungu hawezi kusema uongo, tupate faraja iliyo imara, sisi tuliokimbilia kuyashika matumaini yale yaliyowekwa mbele yetu".

Msomaji, bila shaka umejifunza jambo hapo. Niishie hapa, tukutane tena wiki ijayo. Je, una maoni au kisa cha kimasiha? **Tuma ujumbe kupitia 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Safari ni ndefu mwanamke kuaminiwa kwenye uongozi

MACHI 8, mwaka huu, ilikuwa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo ilifanyika chini ya kaulimbiu ya "Wanawake Katika Uongozi, Chachu ya Kufikia Dunia Yenye Usawa".

Msisitizo mkubwa ulikuwa kuhakikisha idadi ya wanawake kwenye uongozi inaongezeka kutokana na sifa zao na si jinsia na uwepo wao, ni chachu kubwa ya maendeleo na kuleta usawa wa kijinsia.

Pamoja na msisitizo huo, kiuhalisia, bado kuna idadi ndogo ya wanawake katika ngazi za uamuzi yaani kuanzia nafasi za uteuzi, kuajiriwa kwenye taasisi, mashirika, kampuni, serikalini na ndani ya vyumba vya habari.

Mathalani, katika sekta ya habari, bado idadi ya wanawake katika ngazi za uamuzi ni ndogo na si kwamba hawapo wenye uwezo bali ni kwa sababu ya mfumo uliojengeka kiasi cha kukuta uamuzi unafanywa na jinsia moja huku jamii inayolishwa habari ina mchanganyiko wa jinsia zote.

Madhara yake ni kuanzia kukusanya habari na kuzitoa zinakosa jicho la jinsia, kwa kuwa katika habari nyingi wazungumzaji watakuwa wanaume, na inapofika ndani ya chombo cha habari itaonekana kawaida kwa kuwa aliyepokea naye anamtazamo huo huo, huku wanawake wakishindwa kuzungumza wanapotakiwa kufanya hivyo.

Tayari mashirika yasiyo ya kiserikali kikiwamo Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), kinafanya kampeni ya kutambua na kuibua wanawake wenye sifa za kuongoza na wameshafanya mambo makubwa ya mabadiliko katika jamii.

Ikiwa vyombo vya habari ambavyo vina wajibu wa kuelimisha, kukosoa na kuburudisha vitashindwa kufikia usawa wa kijinsia kwa vitendo, maana yake bado jamii ina safari ndefu kuvunja mfumo dume.

Bado vyombo vya habari vinapaswa kujikagua kuanzia habari zinazokusanywa kama zina jicho la jinsia, waandishi wa habari wangapi wanamaliza vyuo na kujiunga na vyombo vya habari na baada ya muda ni wanawake wangapi inabakia kwenye vyumba vya habari.

Nani anawaibua na kuwaamini kuwa wanaweza kuwa viongozi katika vyombo vyao va habari na nafasi nyingine kwenye mashirika, taasisi, kampuni na serikalini na wana nafasi ya kuleta mabadiliko makubwa kupitia kalamu zao, thamani kama hiyo ni lazima itasaidia mabadiliko kuanzia ukusanyanji hadi uchapishaji/utangazaji wa habari husika.

Aidha, katika hotuba yake siku hiyo, Makamu wa Rais, Samia Hassan Suluhu, alisema licha ya Tanzania kufanikiwa kutekeleza maadhimio ya Beijing miaka 25 iliyopita yaliyotoa vipaumbele 12, bado kuna suala la mtoto wa kike, mwanamke na unyanyasaji au udhalilishaji limeendelea.

Suala hili limeshika kasi zaidi tangu ujio wa mitandao ya kijamii ambayo watu wameitumia vibaya kudhalilisha, kujidhalilisha, kuumiza na kuharibu maisha ya wengine kwa kujua au kutojua, hali ambayo inapunguza idadi ya viongozi wanawake.

Kwa sasa licha ya sheria kumlinda mtoto picha za udhalilishaji watoto zinasambazwa kwenye mitandao ya kijamii, jambo ambalo halipaswi kufanyika hivyo linaacha maumivu na huenda lisifutike katika maisha ya mtoto.

Pia, wapo wasichana kwa kutotambua athari za matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii wanarusha picha zao za utupu au wamevaa mavazi ambayo huonyesha sehemu kubwa ya mwili wao na kuwadhalilisha.

Wengine hujipiga picha hizo kwa lengo la kujitangaza kwenye mitandao ya kijamii pasipokujua kesho yao inatengenezwa na leo, kwa kuwa unapokwenda kuomba kazi mahali kinachoangaliwa ni mwenendo wako kwenye mitandao ya kijamii.

Wengine ni wanaume wanaosambaza picha za wanawake kwenye mitandao ya kijamii, ambazo zinadhalilisha utu wa mwanamke ikiwamo kuharibu kesho yake.

Matukio mengine ya ukatili hufanyika ngazi ya familia kwa baadhi ya wanaume kutelekeza mke na watoto, kumpiga mama mbele ya watoto, lugha ya matusi na manyanyaso mengine ambayo hayastahili kutendwa dhidi ya binadamu mwingine.

Mengine ni haki ya elimu ambayo bado ni changamoto kwa baadhi ya makabila watoto wa kike hawaruhusiwi kusoma kwa sababu wanasubiri kuolewa, na wengine walishatolewa mahari.

Mathalani, mikoa ya jamii ya wafugaji bado mtoto wa kike anaandaliwa kwa ajili ya kuolewa, na wazazi hupokea mahari mapema na mwanafunzi hutakiwa kufanya vibaya shuleni ili asiendelee na shule aolewe.

Wako wasichana waliopoteza ndoto zao za maisha kutokana na uamuzi wa wazazi kuwaoza kabla ya kufikisha umri wa kufanya uamuzi, na kuendelea kuwa na wasichana ambao hawajasoma na hawakupata nafasi ya kusoma.

**Tutafakari**



AINA YA KEKI ZILIZOTAMBA KATIKA SHEREHE ZA HARUSI KATIKA MIEZI MIWILI YA MWAKA 2021



# MITINDO




## 'MASSENGER BAG'

## UMARIDADI KATIKA BEGA LAKO

UMESHUHUDIA vijana wa sasa wakibeba mabegi madogo? Basi mabegi hayo yanaitwa 'Massenger Bag', ambayo pamoja na kuwa kama pambo pia humrahisishia mtu kubeba vitu muhimu.

Tena hizi begi hazina bei kubwa, kama jina lake linavyosema 'mkoba wa mjumbe' hazina mbwembwe nyingi kwani ni rahisi kubeba, kufunga na kufungua kwake si jambo gumu.

Kwa kawaida mabegi haya yanatengenezwa kwa kutumia baadhi ya aina ya kifaa asili kama ngozi au vitambaa vigumu, kisha inawekwa mkanda ambao utamfanya mtu kubeba begani au shingoni.

Mtumiaji anakuwa na uwezo wa kuweka kamba yake katika kifua ili begi likae mbele au nyuma.

Mabegi haya si kama yameanza kubuniwa hivi sasa, bali yalianza kutumiwa zamani. Hata hivyo wabunifu wamebuni mitindo tofautitofauti.

Mabegi haya yanafaa si tu kwa matumizi ya ofisini, kama wewe ni mwanafunzi wa chuo pia inaweza ikakusaidia.

Muundo wake imetengenezwa na mifuko midogo ya nje ambayo inakuwezesha kuweka vitu vidogo. Mabegi ya aina hii yanatumiwa na watu wote yaani wanawake na wanaume.

Alafu mabegi ya aina hii hayachagui nguo za kuvaa, zinapendeza kwa vazi la aina yoyote utakaloamua.

UREMBO

# MAAJABU YA PARACHICHI

## Katika kutunza nywele zenye afya



WAPO wanaolalamika kuwa nywele zao hazikui kama inavyotakiwa na pia zinakatika.

Tatizo hilo linawagusa watu wengi kiasi ambacho wanatumia pesa nyingi kutafuta suluhu kwa kununua madawa ya viwandani ambayo mengi yana kemikali hatari.

Imeelezwa na wataalamu kuwa tunda la parachichi linafaa kutibu na kusaidia kwa kiwango kikubwa ukuaji na utunzaji wa nywele.

Wanasema tunda hilo linautajiri wa vitamini E kuliko ile inayopatikana kutoka kwenye mazao ya wanyama pamoja na mayai.

Ndani ya parachichi kuna vitamini B6 ya kutosha, madini ya chuma na potassium kwa wingi. Tunda hili licha ya kusaidia kulainisha ngozi na kuondoa mikunjo, linajulikana kama tabibu halisi wa kulainisha nywele, kusaidia kukua na kuziimarisha na kuzuia kukatika.

**JINSI YA KUFANYA**

Saga parachichi moja mpaka lilainike kabisa. Chukua vijiko vitatu vya asali na kiini cha yai kisha changanya vyote kwa pamoja.

Kabla ya kupaka, osha nywele zako kwa shampoo na uzikaushe kwa kutumia taulo safi.

Paka mchanganyiko huo, kisha kaa nao kwa muda wa dakika 15 halafu osha.

Fanya hivyo mara kwa mara utaona matokeo mazuri katika nywele zako.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# FURAHIA KABICHI YA MAYAI



KABICHI ni aina ya mboga za majani ambayo hupikwa kwa mapishi tofauti.

Unaweza kupika kabichi bila kuchanganya na chochote, pia unaweza kupika kwa kuchanganya na nyama, mayai au chochote unachoona kinafaa kwako.

Leo tutaangalia jinsi ya kupika kabichi iliyochanganywa na mayai, tunaanza na mahitaji pamoja na hatua za kufuata katika upikaji wa mboga hii.

**Mahitaji**

Kabichi moja ya ukubwa wa wastani, mayai manne, mafuta robo lita, vitunguu vinne, karoti kubwa moja, pilipili manga kiasi na chumvi kiasi kwa ladha.

Namna ya kupika

Chukua kabichi ulikatekate kisha uoshe na washa jiko lako la mkaa, gesi au umeme.

Bandika kabichi uliyolikatakata na uache iive kidogo kisha epua.

Menya nyanya, katakata vitunguu, karoti uviweke tayari kwa mapishi.

Bandika sufuria jikoni, kisha weka mafuta ya kupikia, yakipata moto tia vitunguu halafu kaanga mpaka ibadilike rangi na kisha weka nyanya.Nyanya zikishaiva weka karoti kaanga kidogo.

Baada ya hapo weka pilipili manga pamoja na kabichi ulilolichemsha.

Vunja mayai uliyoandaa na kisha changanya na kabichi iliyoungwa tayari na ukoroge hadi mboga yako ikauke.


Mpaka kufikia hapo mboga yetu ya kabichi iliyochanganywa na mayai itakuwa imeiva na tayari kwa kuliwa kwa chakula ukipendacho iwe ugali, wali hata pilau.

Mwisho

# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## HIVI NDIVYO WANAUME WANAVYOPENDA MAZINGIRA NYUMBANI YAWE MUDA WOTE



HIZI ndizo sauti za baadhi ya wanaume wanavyozungumzia kile wanachowafurahisha wawapo nyumbani.

Wanasema baada ya pilika za hapa na pale za kutafuta riziki za familia, nyumbani ndipo huwa mahali sahihi pa kuondoa uchovu huku baadhi wakitumia neno 'kuondoa stress'.

Mwanamume wa kwanza ambaye nilizungumza naye, anasema yeye anapofika nyumbani huwa na picha yake kichwani ya namna anavyotamani kuona mazingira ya nyumba.

"Jioni ile wakati natoka kazini na uchovu wangu, huwa nina picha yangu kichwani kabisa juu ya ambavyo ninatamani nikute nyumba yangu inafanania. Natamani nikifika nikutane na kale ka ubaridi fulani hivi 'amaizing' kanakotoka kwenye pembe tofauti za nyumba yangu ambayo imesafishwa vizuri, "anasema.

"Nikifika kwanza baada ya kuvua viatu vyangu na kuingia sebuleni, nijitupe pwa! kama ishara ya kutua mzigo wa mahangaiko ya kutwa nzima lakini wakati huo huo jicho langu nikilitupa kila pembe ya nyumba nikutane na vitu vya kunifurahisha, namna vitu vilivyopangiliwa kwenye nyumba au jicho langu likiangalia likutane na ua au picha nzuri. Vitu kama hivyo ndiyo nafsi yangu inakuwa kwatuuu, na nasahau shida zote za kutwa nzima," anaongeza.

Mwanamume wa pili, naye anasema huwa anajisikia vizuri anaporudi nyumbani na kukutana na mazingira ya nyumba yakiwa yako katika hali nzuri ya usafi kuanzia ndani na nje.

"Nyumbani raha sana unapoingia unakuta ni kusafi, sebuleni kumepangiliwa vizuri, ukiingia chumbani nako kuko safi, kumesafishwa, kitanda kimetandikwa vizuri kwa ustadi. Hizo ndizo raha zenyewe za nyumbani.

"Ndivyo nyumbani panatakiwa kuwa na si unarudi unakutana na mavyombo yamekaa ovyo, sebuleni nako hakueleweki. Ukiingia chumbani yaani ndiyo usiseme kuko ovyo hakujapangiliwa. Nakwambia nyumbani kwa namna hii huwezi kufurahia kukaa wala kuwahi kuridi," anasema.

Lakini anasema nyumba ikiwa safi na inapangiliwa vizuri kila mahali, lazima mtu atamani muda wote uwepo tu au kutamani kurudi mapema. Nyumbani kunapokuwa kusafi, anasema kunavutia na kunafurahisha na kwamba wanaume wanapenda vitu vya namna hiyo."

Mwanamume wa tatu, anafurahia kuishi nyumba ambayo mara kwa mara hasa ndani anakutana na mabadiliko.

"Yaani aisee mimi nafurahi sana ninapoona mara kwa mara nakutana na mabadiliko kwenye nyumba yangu. Kwa mfano ukirudi unakuta mara makochi yamepangwa kivinge tofauti na ulivyoacha asubuhi au mpangilio wa vitu ndani umebadilika. Raha sana hiyo na kwa namna hiyo nyumbani hapaboi."

00000



# MPANGILIO

## DONDOO MUHIMU YA KUPAMBA BAFU NYUMBANI

**Rangi nyeupe**

RANGI Nyeupe inapendwa duniani kote kutokana na kufanya bafu kung'ara na kuonekana safi kila siku. Inapendeza kuchagua rangi hii kwa sababu watu watakapoingia wanakuwa na furaha zaidi kutokana na usafi wake.

**Ranbgi nyeusi**


Rangi nyeusi inachukuliwa kama urembo unaovutia kwenye bafu, unaweza kuweka marumaru nyeusi na dari ya mchanganyiko. Lakini unatahadharishwa kama bafu ni dogo hakikisha unaweka rangi hiyo baadhi ya sehemu tu ili kupendeza zaidi.

**Rangi mchanganyiko**

Kitaalamu haipendezi bafu kuwa na rangi ya kung'aa sana, lakini unaweza kuchanganya rangi nyekundu ukipamba na bluu.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
'MARA PAAA!!! BONGOFLEVA CHINI, SISI JUU...
DANSI
KAMA UNA-MPENDA MKEO NA UNANIHESHI-MU BABA YAKO... ASOGEE HUKU HARAKA!
JAPO NI MWALIMU MSTAAFU LAKINI NASIKITIKA HUYU SIO MWANAFUNZI!
ANKO ANKO ANKO! SHIKAMOO ANKO...
NIKIITIKIA HUTONIOMBA HELA?
NENDA TU MIE NAPUNGA UPEPO
KWA HIYO UKIITAZAMA LAMI UNAONA BAHARI, NA HIZI GARI NI MELI AU SIO?
ANUSURIKA KWENDA "JELA MIAKA THERA-SINI NA SABA, KWA KOSA LA KUMPIGA MKEWE NA PANGA"
PANGA AU 'KANGA?'
HAYA SASA!!! NATANA NIIONE IKINIONGOZA BAR!
SHOSTI MBONA WEWE SIKU ZOTE UPO SINGO MIMI NNA MUME?
MUMEO HAJANIACHA SINGO
HILI GARI BILA YA KUWEKEWA KIGOGO LINGEKUWA MTARONI.
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...USINYOOSHE MIGUU SHUKA FUPI...

## HABARI KIMATAIFA

# Wengine watatu wauawa Myanmar

**YANGOON, Mynmar**

WAANDAMAJI wengine watatu wameuawa usiku wa kuamkia jana nchini Myanmar, wakati matu walipokaidi marufuku ya kutoka nje usiku.

Kabla ya tukio hilo, mamia ya watu walikusanyika kwa ajili ya kuandaa tukio la kuwasha mishumaa kuwakumbuka watu waliouawa tangu kutokea mapinduzi ya kijeshi. Shirika la Habari la AFP limeripoti kuwa mkanda wa video uliothibitishwa umeonesha miili ya wanaume wawili ambao ni wafuasi wa Chama cha Aung San Suu Kyi. ikiwa imewekwa kwenye nyumba zao na kuzungukwa na maua. Mkanda mwingine ulionyesha polisi wakiwakamata kwa nguvu watu watatu wa mitaa ya mji wa Yangoon, huku wakiwapiga kichwani na kutokomea nao kusikojulikana.

Utawala wa kijeshi ulioipindua serikali ya kiraia na kumkamata Suu Kyi umezidisha matumizi ya nguvu dhidi ya waandamanaji tangu ulipochukua madaraka katika mapinduzi ya Februari Mosi.

Licha ya kutumia mabavu, maelfu ya raia wa Myanmar wameendelea kukusanyika nchini humo kutaka kuachiwa huru kwa Suu Kyi na kurejeshwa kwa utawala wa kidemokrasia

**DW**



Waandamanaji wakikabiliana na polisi wa Mynmar wakati wa maandamano yanayoendelea kupinga hatua ya jeshi kupindua serikali mapema mwaka huu. **(PICHA: THE DAILY STAR)**

# Rais Kenyatta atangaza vikwazo zaidi

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, ametangaza kuongeza kipindi cha marufuku ya watu kutoka nje kati ya saa nne usiku na saa kumi alfajiri kwa miezi mingine miwili.

Aidha, Kenyatta amepiga marufuku mikutano yote ya kisiasa katika kukabiliana na wimbi la tatu la maambukizi ya virusi vya corona nchini humo. Kabla ya tangazo hilo, kiongozi wa upinzani Raila Odinga siku ya Alhamisi, alitangaza kuambukizwa virusi vya Corona siku chache baada ya kuhitimisha mikutano ya kisiasa katika majimbo ya nchi hiyo.

"Ninaelekeza kwamba aina zote za mikusanyiko ya kisiasa imeharamishwa kwa kipindi cha siku 30, kuanzia saa sita usiku," alisema Kenyatta.

Raia wengi wa nchi hiyo walitumaini serikali ingelegeza masharti ili kuendelea na shughuli zao za kawaida, lakini kiongozi huyo alisema jambo hilo halitawezekana.

"Gharama ya uamuzi huu wa ujasiri kwa uchumi wetu ilikuwa kubwa.Lakini faida ya hatua ya haraka ya sera haina kipimo kwa maisha ya binadamu yaliyookolewa" alisisitiza.

Kwa mujibu wa takwimu za serikali, Kenya imepoteza zaidi ya watu 1,879 katika janga hilo.

"Kama hatua isingechukuliwa haraka tungekuwa na maambukizi takriban milioni moja nchini kufikia mwezi Desemba na vifo 150,000. Mifano mingine ilitabiri matokeo mabaya zaidi" Rais Kenyatta aliongeza.

Kenyatta alifichua kuwa taifa limepoteza takriban Sh. bilioni 560 za pato la taifa kutokana na mtikisiko wa uchumi uliosababishwa na janga la Corona

Wakati huo huo, Rais Kenyatta alisema Kenya itaendelea kufanya uamuzi wake kutokana na sera za kisayansi.

"Ushahidi wa mwanzo wa kisayansi kwa mwaka mmoja uliopita umetuonyesha kuwa tunapozidisha vizuizi, viwango vya maambukizi ya jamii vinapungua,"

Kenya imeanza kuwapa chanjo raia wake milioni 1.25 katika awamu ya kwanza inayojumuisha wahudumu wa afya wapatao laki nne na walimu 15,000 katika majimbo yake 47 kwa kutumia dozi milioni 1.02 ya AstraZeneca.

**VOA**

## Umoja wa Mataifa yaonya wanajeshi mamluki Libya

**NEWYORK, Marekani**

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa, imezitaka nchi za kigeni zenye wanajeshi na wapiganaji mamluki nchini Libya kuwaondoa haraka.

Aidha imehimiza kusitishwa haraka kwa mapigano baina ya pande mbili hasimu nchini humo.

Katika taarifa iliyotolewa juzi, Baraza hilo pia limetaka kuheshimiwa kwa vikwazo vya kuingiza silaha nchini Libya ambayo wataalamu wa Umoja wa Mataifa walisema vinakiukwa.

Hata hivyo, chombo hicho kimekaribisha hatua iliyopingwa nchini humo ikiwamo kura iliyopigwa na bunge siku ya Jumatano kuidhinisha serikali ya mpito iliyo na jukumu la kuandaa uchaguzi mkuu uliopangwa mwezi Desemba. Imetoa wito kwa pande zote hasimu kwenye taifa hilo lenye utajri wa mafuta na ambalo limetumbukia vitani tangu mwaka 2011, kuhakikisha zinakabidhi madaraka kwa serikali ya mpito inayoongozwa na waziri mkuu Abdul Hamid Dbeibah.

**DW**

## Familia ya Floyd kulipwa dola mil 27

**MINNEAPOLIS, Marekani**

HATIMAYE baraza la mji wa Minneapolis nchini Marekani, limeidhinisha makubaliano ya kuilipa familia ya George Floyd kiasi cha dola milioni 27.

Uwamuzi wa kuilipa fidia familia hiyo umefanyika karibu mwaka mmoja tangu Mmarekani huyo Mweusi alipouawa kutokana na hujuma za polisi.

Tangazo hilo lilitolewa na meya wa mji huo, Jacob Frey, katika mkutano na waandishi habari uliohudhuriwa pia na ndugu wa Floyd pamoja na wanasheria wa familia yake. Kiasi hicho cha fedha ni kikubwa zaidi kuwahi kulipwa kwa familia za wahanga wa matendo ya jinai yanayofanywa na polisi.

Kutokana na malipo hayo, inaondoa uwezekano wa familia ya Floyd kufungua kesi mahakamani.

Floyd alifariki dunia Mei mwaka jana baada ya polisi mmoja mzungu kumkandamiza kwa goti shingoni kwa zaidi ya dakika nane katika tukio lililorekodiwa na mpita njia.

Kifo chake kilizusha hasira na maandamano makubwa nchini Marekani na duniani kote kulaani matendo ya ukatili wa polisi dhidi ya watu weusi.

**DW.**

SAFU

## MAKALA

# Elimu pekee haikufanyi kuwa kiongozi bora



Na Magabilo Masambu

**Uongozi unahitaji hekima na busara, mambo haya hakuna mahali yanasomewa, unapokuwa shuleni zaidi unajifunza ustaarabu, lakini ukiwa na hekima na busara unaposoma unapata ujasiri zaidi wa kuzieleza wazi.**

ELIMU ni nyenzo muhimu katika maisha ya mwanadamu. Hata maandiko ya dini yanasema mshikeni elimu wala msimwache aende zake. Hii inadhihirisha jinsi gani elimu ina umuhimu mkubwa katika harakati za mwanadamu duniani.

Kazi mojawapo ya elimu ni kumjengea mtu ujasiri wa kujiamini kwamba amesoma na anaweza kufanya ama yale aliyoyasomea au yenye kufanana na hayo. Kujiamini huko ndiko mara nyingi huwafanya baadhi ya watu wanapotaka nafasi za madaraka, kutanguliza sifa walizonazo katika elimu, kueleza namna gani watatekeleza majukumu hayo iwapo watazipata nafasi hizo.

Ni kweli kwamba elimu inaweza kukupatia nafasi ya uongozi, lakini kitakachoamua udumu au usidumu katika nafasi yako hiyo ni tabia zako binafsi pamoja na mambo mengine. Kuwapo kwa sababu nyinginezo zinazoamua uendelee au usiendelee ni ushahidi tosha kwamba elimu pekee haiwezi kukufanya ukawa kiongozi bora japo inaweza kukufanya ukawa kiongozi.

Wako wanaoamini kwamba uongozi husomewa, lakini kinachosomewa ni taratibu za kuongoza si uongozi wenyewe kwa sababu uongozi unajumuisha mambo mengi yaliyoko vyuoni na yasiyokuwapo. Si kila jambo linalohusu uongozi linapatikana shuleni, mengine yanategemea maisha katika jamii husika pamoja na mambo ya mila na desturi.

Ni dhana potofu kuamini kwamba elimu uliyonayo, inaweza kukufanya ukawa kiongozi bora na kwamba utakuwa wa kuiwa mfano. Kama elimu ingekuwa kigezo cha kumfanya mtu awe kiongozi bora, basi wenye elimu zinazofanana wasingekuwa wanatofautishwa katika utendaji wao.

Maana yangu ni kwamba, mwanafunzi X na Y waliosoma darasa moja na mwaka mmoja pale chuo kikuu cha Dar es salaam kitivo cha sayansi ya siasa, kama elimu ni uongozi basi tungetegemea mtazamo wa jamii juu yao, uwe ni unaofanana. Lakini cha ajabu utasikia watu wanasema yule ni kiongozi mzuri kuliko huyu.Tafasiri yake kuna vitu fulani mmoja anavyo mwingine hana, hivi vinatokana na mambo yaliyo nje ya elimu.

Uongozi unahitaji hekima na busara, mambo haya hakuna mahali yanasomewa, unapokuwa shuleni zaidi unajifunza ustaarabu, lakini ukiwa na hekima na busara unaposoma unapata ujasiri zaidi wa kuzieleza wazi.

Ukiwa huna hekima na busara ukapata elimu, unaweza kujikuta unafanya vitu ambavyo vinawashangaza hata wale wasiokwenda shule na kuhoji kuhusu elimu yako. Kuna wakati fulani unaweza kuwa kwenye mkutano, akasimama mtu mmoja akatoa hoja kila mtu akajiuliza kiwango cha elimu yake. Hii inamaanisha kwamba elimu haitakiwi kuonekana katika makaratasi, bali katika fikra.

Uongozi ninaouzungumzia hapa si wa kisiasa tu, bali wa mahali popote ilimradi wewe ni kiongozi. Unaweza kuwa benki, mahakamani, kanisani, shuleni, kwenye shirika, serikalini, jeshini au mahali popote palipo na watu wa kuongoza na kuongozwa.

Uongozi haukuanza baada ya uanzishwaji wa mfumo rasmi wa elimu, badala yake hata kabla ya elimu hii palikuwapo na viongozi katika mifumo mingine ya uongozi na huu ni ushahidi mwingine kuthibitisha kwamba elimu tulizonazo si kigezo pekee cha kupata nafasi za uongoza.

Iko minong'ono mitaani watu wanasema wasomi wa siku hizi ndiyo hufanya mambo ya ajabu zaidi kuliko wasiokwenda shule. Kama hilo ni kweli maana yake hayo mambo ya ajabu yanaweza pia kufanywa katika nafasi za uongozi.

Eneo moja linaloonekana kulalamikiwa kutokana na elimu yetu ni malezi. Yako maneno yanazungumzwa mitaani na si ya kupuuza kwamba wasomi tunalea watoto wetu vibaya na kama tumepata elimu lakini tukalalamikiwa katika eneo la malezi, maana yake uongozi unatushinda kutokea kwenye familia.

Tusiibebe elimu yetu katika nafasi zetu za uongozi, bali elimu itubebe katika utendaji wetu. Tusiitafsiri elimu kama uongozi, bali uongozi wetu uonyeshe kiwango cha elimu tulichonacho kwa vitendo.

Simaanishi watu wasisome kwa sababu tu elimu si uongozi, bali kutoitumia elimu kama ngao au silaha ya kuhalalisha uongozi bora. Lakini pia lazima kufahamu kwamba uongozi pia ni karama.

Upande wa pili makuzi na malezi pia yana nafasi katika kumjenga mtu awe kiongozi bora. Ushirikiano wake na wengine toka utoto ulikuwaje? Alilelewaje? Matatizo ya wengine huyatazamaje? Je, ni mtu anaezingatia sheria, taratibu na kanuzi za eneo la kazi? Mwisho elimu isiwe kichaka cha wasio na karama ya uongozi kujifichia.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Michezo ya sarakasi, kuendesha ringi imeishia wapi?



Na Adam Fungamwango

**Lakini yote heri tu. Kila kitu na zama zake. Na kila walichokifanya na wanachofanya sasa kina faida na hasara zake. Maisha yale ya watoto wa zamani yalikuwa na faida na hasara zake na hata hawa wa sasa pia.**

KUMEKUWA na mijadala mbalimbali mitaani na kwenye mitandao ya kijamii kuhusu maisha ya watoto wa zamani na wa sasa.

Wengine wanadai watoto wa zamani akili zao zilikuwa hazipevuki mapema lakini walikuwa watundu, wathubutu na majasiri na wenye uwezo wa kufanya au kujaribu vitu mbalimbali hata vile vilivyoonekana vya hatari.

Wa sasa wana akili sana. Tena wanakuwa na akili wakiwa bado wadogo mno kutokana na kukua kwa teknolojia. Tatizo ni kwamba watoto wa sasa ni goigoi. Hawana uthubutu, waoga na wanapenda vitu rahisi.

Ndiyo maana tunaona wengi wao badala ya kutafuta viwanja wa kucheza soka, wanashinda kwenye vyumba vya kucheza gemu. Mpira unachezwa kwenye gemu badala ya uwanjani. Inasababisha nchi kwa miaka ya sasa na ijayo kukosa wachezaji wenye vipaji vinavyoanzia ututoni kwenye misingi ya soka.

Kwa sababu wanaanzia kucheza ukubwani. Ututoni ni gemu tu.

Mtoto wa sasa asubuhi unaweza kumvalisha shati na kaptula, ukampaka mafuta na kumvisha viatu au kandambili akarejea mchana yuko hivyo hivyo.

Tofauti na watoto za zamani. Ukimvalisha hivyo, mchana akirudi unaweza ukamsahau. Atakuwa na vumbi. Shati limechafuka. Amepauka kama kipande cha mhogo mkavu. Kibaya zaidi unaweza pia ukakuta kiatu kimoja au kandambili amepoteza. Au vyote pea nzima imepotea.

Lakini yote heri tu. Kila kitu na zama zake. Na kila walichokifanya na wanachofanya sasa kina faida na hasara zake. Maisha yale ya watoto wa zamani yalikuwa na faida na hasara zake na hata hawa wa sasa pia.

Leo tunajikumbusha purukushani ya michezo ya watoto wa zamani ambayo ilikuwa inasababisha warudi nyumbani wako hoi. Pamoja na kucheza soka, kuna michezo fulani ya hatari walikuwa wanaifanya hasa watoto wa mijini, hususan Dar es Salaam. Kudandia magari.

Watoto wa zamani walikuwa jasiri na kufanya mambo ya hatari kwa kudandia magari ambayo yalikuwa yanapita au kusimama hasa yakiwa yanatembea taratibu.

Wanadandia halafu baadaye wanashuka kwa namna ya kujiachia kutoka kwenye gari linalotembea.

Mungu bariki mara nyingi walikuwa wameshajua namna ya kushuka. Nadhani walikuwa wanafundishana. Lakini mara chache baadhi walikuwa wanakosea na kuanguka. Hii ilisababisha baadhi kupata majeraha.

Watoto wengi wa zamani miaka ya 1960, 1970 hadi 1980 na hata 1990 walikuwa watundu mno. Wengi walijifunza sarakasi.

Ni mchezo mmoja wa hatari, lakini ulikuwa unapendwa mno na watoto ambao walikuwa wakishindana, kila mmoja akionyesha uhodari wake na kuruka 'soti' vizuri, kiufundi na kwa mbwembwe zaidi kuliko wenzake.

Wenyewe wanasema hii iliwafanya watoto wengi wa zamani kuwa fiti mno, kiasi kwamba hata magonjwa mengi yaliwapita kando.

Mbali na mchezo huo, kulikuwa na kujiviringisha kwenye magurudumu. Katikati ya gurudumu ambalo halipo kwenye gari kunakuwa na duara kubwa hivi. Mtoto mmoja akajikunja pale, halafu wenzake wanaliendesha huku yeye akiwa ameng'angania pale akizunguka kama gurudumu lenyewe.

Ukiacha hilo kuna kuendesha ringi. Ni lile lililopo katikati ya tairi la basikeli. Watoto wengi walikuwa na maringi. Na Uendeshaji wenyewe ulikuwa ni kutafuta mti au waya, ukipachikwa katikati ya ringi.

Watoto wa zamani walikuwa wanapenda sana kuendesha kwa sababu huwafanya kukimbia. Wakati mwingine kurahisisha safari za kutumwa huku na kule na wazazi wao. Kwenda dukani, kumwita mjomba, shangazi au baba mdogo kijiji kingine walitumia sana ringi na kurejea baada ya muda mfupi.

Kuna mchezo pia wa kusereреka kutoka sehemu za kilimani na kwenda bondeni. Ni mchezo uliokuwa unachana sana nguo za watoto hasa kaptura.

Pamoja na kwamba ilikuwa burudani kwao, lakini hili lilikuwa zoezi tosha kwa watoto wa kipindi hicho. Yaliwafanya kuwa na afya bora, kuwa wepesi.

Kujiamini na kuifanya akili yao kufikiria kwa haraka zaidi.

Inawezekana kabisa hii ilisababisha watoto wengi wa zamani kuwa na uwezo mkubwa wa kubuni vitu mbalimbali, ikiwemo kujitengea wakiwa bado na umri mdogo tu.

Ni aghalabu kwa sasa kumkuta kijana hata mwenye miaka 22 hivi ameondoka kwa wazazi wake, lakini wakati huo, miaka 18 tu anaweza kuwaacha wazazi wake na kwenda kutafuta maisha, tena mkoa mwingine mbali na hapo alipozaliwa.

Achilia mbali michezo hiyo. Kulikuwa na michezo ya kuzungusha kitufe, bila kusahau mchezo wa kurusha tiara, ambao wakati huo watoto waliita kishada. Aliyekuwa na uwezo wa kurusha na kwenda juu na mbali zaidi ndiye anayeonekana kama mshindi.

Hizi ni baadhi ya burudani zilizotikisa mno enzi hizo.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risasi ziliwafanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu. Haikuwa hivyo. Yeyote aliyedhani ni majambazi alikosea. Aliteremka mtu mmoja kwenye gari na alichofanya ni kumpora mwanamke aliyekuwa kwenye kituo cha basi mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini amepora mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji?

# Nina Jambo Langu-13

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

NAONA hapa kila mtu ananilaumu mimi. Na mimi ndiyo naonekana mkosaji ninayestahili kuadhibiwa kwa kupewa talaka kwa sababu ya kutekwa kwa huyu mtoto na jinsi alivyopatikana. Naonekana sikuwa mwanimifu kwenye ndoa. Kila mtu anadhani kuwa aliyemteka Diana ni hawara yangu ndiyo maana amerudishwa kirahisi, eti mimi nimekwenda kumwomba kwa kulinda ndoa. Hii si kweli." Neema aliendelea kuiambia hadhara.

Maneno aliyokuwa anaongea tayari yalikuwa yameshazoeleka. Ndiyo ambayo yamesababisha apewe talaka. Yalianza kuwachosha waliohudhuria. Wao walidhani kuna kipya ambacho hawakijui. Walitaka amalize akusanye virago vyake na wao kila mmoja aende kwenye shughuli zake.

"Baba Diana majuzi alinitaka nimtaje mtu ambaye alimteka mtoto. Sasa leo hii namleta kabisa hapa hapa aliyemteka mtoto huyu. Sasa kama mtamkamata sawa au sijui mtaelewana naye vipi mtajua wenyewe." Ni maneno ambayo yalimshtua kila mtu.

Kwa jinsi walivyofikiria. Hakuna hata siku moja walioamini hata kumsikia, achilia mbali kumuona mtu huyo aliyemteka mtoto.

"Utamleta kwenye kikao kijacho au?" Aliuliza mmoja wa wanandugu.


"Hapa hapa, ameshafika yupo nje hapo."

Kila mmoja sasa alipigwa na mshangao, pamoja na mshawasha wa kutaka kujua nini kinaendelea. Mtekaji kujileta, tena kwenye kikao ambacho ndugu wote wamekusanyika, lilikuwa jambo la kufikirika zaidi na si la kiuhalisia.

Kila mtu sasa damu ilimchemka akitaka kumwona mtu aliyemteka mtoto huyo ambao wote waliamini ni hawara wa Neema.

Alichofanya Neema ni kusimama na kwenda kufungua mlango ili kuelekea kwenye geti lao dogo kumfungualia mgeni.

Mgeni wa ajabu. Mgeni mtekaji. Mtekaji ambaye ameamua kujileta nyumbani kwa mtoto aliyemteka. Mtekaji asiyeogopa kukamatwa.




**Tayari waliona kuna kitu zaidi ya kile ambacho wanakifahamu wao. Kuna fumbo zaidi ya lile wanalolijua. "Karibu wifi." Mmoja wa dada wa Ben alimkaribisha.**

Mtekaji aliyeamua kwenda moja kwa moja kwenye kikao cha familia cha ndugu wa wazazi wa mtoto aliyetekwa. Mtekaji ambaye ameitwa na mama wa mtoto aliyetekwa.

Yeyote aliyedhania aliyeingia ndani alikuwa mtekaji mwanamume alikosea. Aliyeingia alikuwa mwanamke. Alikuwa ameshatimiza umri wa miaka 30 hivi. Pamoja na umri huo, urembo bado ulimng'ang'ania. Kasoro ndogo aliyoonekana nayo ni alishaanza kuuachia mwili wake.

Alionekana mnene kuliko miaka kadhaa iliyopita.

Kila mmoja aliyekuwa ndani alionekana kushtushwa na mgeni hiyo. Unaweza kudhani walishtuka kwa sababu walidhani ni mwanamume baada ya kuambiwa anayekuja ndiye mtekaji.

Unaweza kudhani kuwa walishtuka kwa sababu tu aliyeingia ni mwanamke na wao walidhani ni mwanamume. Hapana.

Kikubwa ni kwamba alieyeingia ndani hakuwa mgeni sana kwa asilimia 80 ya waliokuwa kwenye mkutano huo. Ni Ester.

Tayari waliona kuna kitu zaidi ya kile ambacho wanakifahamu wao. Kuna fumbo zaidi ya lile wanalolijua.

"Karibu wifi." Mmoja wa dada wa Ben alimkaribisha.

"Hiki jamani si tulisema ni kikao cha familia? Mbona kama naona wanakuja watu wengine ambao hawahusiki." Ilikuwa ni sauti ya Ben ambaye wakati akiongea hayo alisimama na kutaka kutoka.

Ni mjomba wake ndiye aliyemuamuru arejee na kuketi pale alipokuwapo.

"We, usitufanye sisi wajinga. Tumeacha kazi zetu tumekuja huku kukusikilizeni ninyi na upuuzi wenu. Hebu tusikilize kila kitu na kila mtu halafu tutatoa uamuzi wa jumla, sasa kuanza sijui fulani atoke, sijui nini hii ina maana gani?

"We umempa talaka mke wako umesema amekabidhiwa mtoto na watekaji bila kukushirikisha na ukasema mtekaji alikuwa mwanamume na una wasiwasi kuwa huenda walikuwa na uhusiano. Ukatuambia pia utekaji huu huenda una dalili za kudaiana mtoto na mpenzi wake huyo.

"Sasa yeye kakataa na kamleta mtu ambaye anasema ndiye aliyefanya hivyo. Aliyekuja hapa sisi wote tunamfahamu. Ni mama Tina huyu. Inawezekana kuna kitu ambacho hatukifahamu hapa." Ilikuwa sauti ya mjomba ikinguruma.

Ben alirejea na kukaa. Lakini alionekana kama mtu mwenye wasiwasi hivi.

"Habari za siku nyingi shemeji zangu, wifi zangu na wakwe zangu. Samahani sana, mimi nimekuja hapa kama mgeni tu mwalikwa. Sikuja kama mwanandugu. Hapa mimi nimekuja kwa nia tu ya kumtetea rafiki yangu au shoga yangu Neema au mama Diana.

Ukweli ni kwamba aliyemteka mtoto wenu Diana wala si hawara yake kama wengi mlivyokuwa mnadhani. Aliyemtemka ni rafiki ya mjomba wangu. Jina siwezi kuwatajia na hii ni baada ya kusimuliwa kisa kizima nilichofanyiwa na Ben. Nia haikuwa mbaya. Nitawaambieni tu.

"Wote mnafahamu hapa kuwa Ben ndiye mume wangu ambaye alinioa kwa ndoa ya kanisani ambapo wengi wenu hapa mlihudhuria.

Alichonifanya Benson ilikuwa baada ya kumzaa Tina tu, akaanza kutoonekana nyumbani, kulala nje, kurudi usiku na siku isiyo na jina akaondoka moja kwa moja."

Maelezo yale yalionekana kuwaingia wote waliokuwa kwenye mkutano huo.

Wote wanachofahamu hapo ni kwamba Ben alitengana na mzazi mwenzake kwa sababu alimfumania ndani na mwanamume mwingine. Tena waliambiwa walikuwa wanafanya hivyo, wakati mtoto bado mchanga kabisa, kitu kilichowakasirisha ndugu wote.

Ndivyo Ben alivyowadanganya ndugu zake, akamkimbia Ester kwenda kuishi kwingine. Zote hizo zilikuwa kutafuta sababu. Tayari alishampata mwanamke mwingine Neema.

Kukacha kurudi nyumbani au kuchelewa, alikuwa anakwenda kwa Neema alikompangia chumba. Akaionja asali akataka kuchonga mzinga. Akamtengenezea hilo zengwe la kumfumania ili kupata uhalali kutoka kwa ndugu zake, akahamia moja kwa moja kwa Neema na kumtelekeza kabisa Ester akiwa na mtoto mchanga. Wakafunga ndoa ya kiserikali na Neema.

"Labda kuna kitu aliwadanganya. Ukweli ni kwamba alinitelekeza na mtoto nikiwa na mtoto mchanga Tina na kwenda kuona mwanamke mwingine." Alisema na kuwaangalia jinsi watu walivyokuwa wakisikiliza kwa makini, wakiwa kama hawaamini kile alichokuwa anaongea.

"Iliniuma sana. Nilikuwa simjui mwanamke huyo ni nani. Kumbe ni huyu hapa aliyenialika, Neema."

INAENDELEA JUMAPILI



# ATAKAYEMPATA MBWA WA WEMA KULAMBA MIL 2

STAA wa filamu za Bongo Muvi, Wema Sepetu, ametangaza donge nono la Sh. Milioni moja kwa mtu atakayefanikiwa kumpata mbwa wake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Wema amesema mbwa wake anayeitwa Vanilla au Manunu ambaye ni kama rafiki yake wa karibu, alipotea jana na hivyo amekuwa katika wakati mgumu.

"Mbwa wangu amepotea, kwa yeyote atakayemuona popote please anijulishe kuna zawadi ya Milioni 2, amepotea asubuhi hii(jana), naomba mnisaidie 'please guys help me' anaitwa Vanilla au Manunu amevaa kigauni cha brown".



# J. LO AMTEMA MPENZI WAKE

MWANAMUZIKI wa Marekani, Jennifer Lopez maarufu kama J. Lo, ameachana rasmi na mpenzi wake Alex Rodriguez.

Mwimbaji huyo wa kibao cha "Love don't cost a thing" na Rod wameachana baada ya kuishi pamoja kwa kipindi cha miaka minne.

J.Lo na A. Rod, walianza uhusiano wao mwaka 2017, na kuvalishana pete ya uchumba mwaka 2019.

Alex Rodriguez amepost picha mapema akiwa Miami kwenye Yacht akisema "Hakuna kujali, nijiselfie, nini umepanga mwisho wa wiki hii? Mara ya mwiSho kuposti picha wakiwa pamoja ilikuwa ni Februari 28 mwaka huu.

## Giny Babah atabiri mastaa hawa 'Wataachana'

MSANII anayekuja kwa kasi katika muziki wa Bongo Fleva, Joshen Adam, maarufu kama 'Giny Babah' yupo mbioni kutambulisha kibao chake kipya hivi karibuni.

Akizungumza na Gazeti hili, Giny Babah amesema wimbo huo unaoitwa 'Wataacha' utakuwa hewani siku chache baada ya kukamilika kutengenezwa katika studio ya Kazo Beats ya jijini Dar es Salaam.

"Meneja wangu Yaso BM anafanya kila juhudi kuhakikisha ngoma inatoka hivi karibuni na kuwapa mashabiki wangu kile wanachopenda. Mwendo utakuwa bandika bandua hadi kitaeleweka," amesema Giny.



## HABARI MICHEZO



# DI MARIA ASAINI MKATABA MPYA

**PARIS, Ufaransa**

ANGEL Di Maria amesaini mkataba mpya wa mwaka mmoja zaidi na Paris Saint-Germain.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 33, amekubali kusaini mkataba huo utakaomweka klabuni hapo hadi mwishoni mwa msimu ujao, huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja.

Di Maria ameshinda mataji 16 akiwa na PSG tangu alipojiunga kutoka Manchester United mwaka 2015 kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 63.

Katika mechi 248 alizocheza kwenye mashindano yote, kiungo huyo amefunga mabao 86 na kutoa pasi za mwisho 99.

Akizungumza mwezi uliopita, Mkurugenzi wa Soka wa PSG, Leonardo alithibitisha Di Maria ni mmoja wa wachezaji muhimu ambao wataongezewa mkataba pale PSG.

Wengine ambao wapo kwenye mipango ya kupewa mikataba mipya ni Kylian Mbappe na Neymar.

Di Maria amecheza mechi 27 kwenye mashindano yote msimu huu, akifunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho 10.

# CHELSEA YAJIANDAA KUMSAJILI COMAN




**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imeingia kwenye anga za kumsajili winga wa Bayern Munich, Kingsley Coman mwenye umri wa miaka 24, katika dirisha la usajili la majira ya joto.

Coman anahusishwa kujiunga Chelsea baada ya tetesi kumtaja winga wa klabu hiyo, Christian Pulisic kutaka kuondoka baada ya kukosa nafasi katika kikosi hicho kutokana na majeraha ya mara kwa mara.

Coman ana thamani ya Euro milioni 55 katika soko la usajili ambayo inatajwa kuwavutia zaidi Chelsea kulinganisha na bei za wachezaji wengine walioko sokoni katika kipindi hichi kuwa juu.

Coman amecheza jumla ya mechi 25 msimu huu katika mashindano yote akiwa na Bayern Munich, akiwa amefunga magoli sita na kutoa pasi za mwisho 11.

Mkataba wa sasa wa Coman unaisha Juni, mwaka 2023 na inasemekana Bayern Munich wanapata shida kumwongeza mkataba mpya kutokana na kupanda na kushuka kwa kiwango cha mchezaji huyo.

# RONALDO ANATAKA KUREJEA MADRID


**MADRID, Hispania**

CRISTIANO Ronaldo anataka kurudi Real Madrid, kwa mujibu wa gazeti la Diario AS la jana Jumamosi.

Baada ya kukaa kwa misimu miwili kule Juventus, sasa Ronaldo anaona ni wakati mwafaka kwake kurudi Real Madrid, hasa baada ya kibibi kizee hicho cha Turin kutolewa **kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ronaldo ambaye ni mfungaji wa wakati wote wa Madrid ameripotiwa kwamba, hataki tena kuendelea kucheza kule kwenye viunga na Turin na ndoto yake ni kurudi Santiago Bernabeu.**

Majaliwa ya Ronaldo na Juventus yamekuwa shakani baada ya kutolewa mapema kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ikiwa ni kwa msimu wa pili mfululizo.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, ambaye aliondoka Madrid na kwenda Juve mwaka 2018, ameripotiwa kuwasiliana na Los Blancos hao kwa miezi kadhaa.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# AGUERO AKANUSHA KUJIUNGA NA BARCA

Asema yeye bado ni mchezaji wa City na amewataka wanaovumisha kutulia na kuacha tetesi...

**MANCHESTER, ENGLAND**

NYOTA wa Manchester City, Sergio Aguero, amekanusha uvumi wa kuhamia kwa miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Barcelona.

Aguero mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na mfungaji huyo wa wakati wote wa City bado hajasaini mkataba mpya na vinara hao wa Ligi Kuu England.

Kumekuwa na uvumi kwamba, Aguero amefikia makubaliano ya awali na rais wa Barca, Joan Laporta ili kwenda kujiunga na rafiki yake, Lionel Messi kwenye Uwanja wa Camp Nou.

Aguero, ambaye amekuwa akikumbwa na majeruhi ya mara kwa mara na kujikuta kwenye wakati mgumu wa kupenya kwenye kikosi cha kwanza cha Kocha, Pep Guardiola msimu huu, amejibu uvumi huo.

"Wote wanaandika Barca, Barca, Barca," amesema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 raia wa Argentina kupitia Twitch.

"Hebu tutulie, tuangalie. Acheni. Bado nipo na City."

Sasa ni miezi 13 na nusu tangu Aguero ambaye anashika nafasi ya nne kwa wafungaji wa wakati wote kwenye Ligi Kuu England, alipofunga bao lake la 180.

Majeruhi ya mara kwa mara yakamfanya afanyiwe operesheni msimu wa 2019-20 na hajawa na muda wa kutosha kucheza.

Aguero alitokea benchi wakati Manchester City wakishinda mabao 5-2 dhidi ya Southampton, akicheza kwa dakika 18 za mwisho, Jumatano.

City wanaongoza kwa pointi 14 kileleni mwa msimamo dhidi ya majirani zao Manchester United.

## KWA UFUPI

### FELIX ANUKIA UNITED
MANCHESTER City inafikiria kumsajili straika wa Atletico Madrid, Joao Felix mwenye umri wa miaka 21 raia wa Ureno, kama mrithi wa Sergio Aguero, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Eurosport)***

### HAALAND AKARIBIA CITY
MANCHESTER City wanaongoza kwenye mbio za kumwania mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20. ***(Mail)***

### BARCA YAJIIMARISHA
BARCELONA wamemfanya Erling Haaland mwenye miaka 20 kuwa chaguo lao namba moja kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto. ***(Mundo Deportivo)***

### BABA MESSI VS BARCA
BABA mzazi wa Lionel Messi anapanga kusafiri kwenda Barcelona kesho Jumatatu ili kujadili majaliwa ya nyota huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 33. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### RONALDO KURUDI MADRID
WAKALA wa Cristiano Ronaldo, Jorge Mendes, amezungumza na Real Madrid kuhusu uwezekano wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 raia wa Ureno kurudi pale Bernabeu kutoka Juventus. ***(El Chiringuito, via Marca)***

### NEYMAR, PSG WATETA
MAZUNGUMZO kati ya fowadi wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 29 na Paris St-Germain kuhusu mkataba mpya yanaendelea. ***(Le10 Sport - in French)***

### DE GEA AWEKWA SOKONI
MANCHESTER United itasikiliza ofa kwa golikipa wake raia wa Hispania, David de Gea mwenye umri wa miaka 30. ***(Football Insider)***

### CAVANI HAKIELEWEKI
MANCHESTER United bado haijui hatima ya straika wake, Edinson Cavani raia wa Uruguay mwenye umri wa miaka 34. ***(Manchester Evening News)***

### UNITED, CHELSEA VITANI
MANCHESTER United na Chelsea zote zinawaniwa kumsajili mlinzi wa AS Roma na Timu ya Taifa ya Italia, Gianluca Mancini mwenye umri wa miaka 24. ***(Express)***

### DELORT AWA LULU
RAIS wa Montpellier, Laurent Nicollin mwenye umri wa miaka 29, anamatumaini ya kumshawishi straika wa Algeria, Andy Delort mwenye umri wa miaka 29, ambaye pia alihusishwa na Newcastle United na Wolves. ***(Midi Libre, via Team Talk)***

### GALLAGHER SOKONI
KLABU ya Crystal Palace bado inamwania kiungo, Conor Gallagher mwenye umriwa miaka 21. ***(Football London)***



# SIMBA QUEENS KAMBINI KUIWINDA ALLIANCE GIRLS

**Na Shufaa Lyimo**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens, wanaingia kambini leo kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wao unaofuata dhidi ya Alliance Girls utakaochezwa Machi 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' alisema kikosi hicho kitaanza mazoezi rasmi kesho kwa ajili kujiweka tayari kwenda kuwakabili wapinzani wao ambao pia wamekuwa na wachezaji wenye uzoefu.

Mgosi alisema kwake kila mechi ni sawa na fainali na anaamini kiwango walichokionyesha katika mchezo uliopita dhidi ya watani zao Yanga watakiendeleza.

"Baada ya kumaliza mechi dhidi ya Yanga Princess, ligi ilisimama kwa muda wa wiki mbili, kwa upande wangu nitaanza maandalizi ya mchezo huo Jumatatu," alisema kiungo huyo wa zamani wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba.

Kocha huyo alisema anaupa umuhimu na heshima mchezo huo dhidi ya Alliance Girls kwa sababu anaamini wapinzani wao wanacheza soka la ushindani.

"Si timu ya kuidharau, inafahamu namna ya kujipanga na kuzuia mashambulizi, tutakwenda Mwanza kwa tahadhari, malengo yetu yako pale pale kuchukua ubingwa, hivyo kila mechi kwetu ni sawa na fainali," Mgosi alisema.

Aliongeza amewaandaa wachezaji wake kupambana katika kila mchezo ili malengo ya kuondoka na pointi tatu yatimie na kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Tuna muda mrefu wa kujiandaa na kurekebisha pale kwenye upungufu, lakini naendelea kuwashukuru mashabiki wetu ambao wamekuwa wakitupa ushirikiano wakati wote tunapokuwa na mechi, hii inatuongezea nguvu ya kupambana ili kuwapa furaha," alisema Mgosi.

Simba Queens yenye pointi 39 baada ya kucheza mechi 15 inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti ikifuatiwa na Yanga Princess yenye pointi 38 wakati ES Unyanyembe ambayo haina pointi hata moja ikiburuza mkia.




Mshambuliaji wa Mbuni FC ya Arusha, Salum Haji (kushoto), akiwatoka wachezaji wa Pan African katika mechi ya Kundi A Ligi Daraja la Pili Tanzania Bara, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Pan African ilishinda mabao 5-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hitimana kuendelea kuula Mtibwa

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya Mtibwa Sugar kutokuwa na matokeo mazuri katika mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea nchini, uongozi wa Mtibwa Sugar umesema bado wana imani na kocha wao, Hitimana Thiery, imeelezwa.

Mtibwa Sugar, haijashinda mechi yoyote ya Ligi Kuu Tanzania Bara tangu kuingia kwa mwaka 2021, imecheza mechi tano, imetoka sare tatu na kufungwa michezo miwili.

Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, aliliambia gazeti hili bado wanaamini Hitimana ana uwezo wa kuivusha timu hiyo katika sintofahamu waliyopo tofauti na baadhi ya wadau wa soka wanavyofikiria.

Kifaru alisema kocha huyo raia wa Rwanda ameikuta timu hiyo ikiwa kwenye mazingira ambayo si mazuri na tayari ameshaanza kuijenga licha ya matokeo kuendelea kuwa mabaya.

"Pamoja na matokeo mabaya tunayoendelea kuyapata, lakini klabu ya Mtibwa Sugar bado tuna imani na kocha wetu. Yeye ameikuta timu ikiwa kwenye mazingira ambayo si mazuri kwa hiyo si rahisi akapata mafanikio haraka. Ni lazima tumpe muda, tunajua ni mwalimu bora, tuna imani tukikaa naye kwa muda mrefu atabadilisha," alisema Kifaru.

Kauli hiyo, inafuta wasiwasi uliopo kwa mashabiki kuwa huenda kocha huyo naye akaonyeshwa mlango wa kwaheri kama ilivyokuwa kwa watangulizi wake, Mecky Maxime na Zuberi Katwila.



## Wadau wamlilia Katibu FA Iringa

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imetangaza kwa masikitiko kifo cha Kamisaa wa ligi na Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Mkoa wa Iringa (IRFA), Dk. Ally Ngalla kilichotokea juzi usiku mkoani humo.

Mwenyekiti wa TPLB, Steven Mnguto, alisema kufuatia kifo cha Ngalla, amewaagiza wasimamizi wa mechi zote zilizotarajiwa kucheza jana hapa nchini, kusimama dakika moja ya maombolezo kabla ya kuanza kwa mchezo.

"Kifo cha Dk. Ngalla kimeacha pengo kubwa katika familia ya mpira wa miguu kutokana na utendaji wake wa kazi uliowavutia wadau wengi nchini,...Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi," alisema Mnguto.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), Lameck Nyambaya, alisema katika taarifa yake Dk. Ngalla alikuwa ni nguzo muhimu katika kuimarisha na kuendeleza uhusiano mzuri baina ya Iringa na mikoa mingine.

Katika kipindi cha kuanzia Januari, mwaka huu Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limepoteza makatibu wengine wawili, Vicent Majili aliyekuwa akiiongoza Njombe na Hamisi Semka wa Morogoro (MRFA).

## Umakini waitesa Kipanga Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa Kipanga, Rashid Lato, amesema sababu kubwa timu yake kupoteza mchezo wa tatu mfululizo katika Ligi Kuu Zanzibar ni wachezaji kukosa umakini.

Lato aliliambia gazeti hili jana tangu kuanza kwa mzunguko wa lala salama wa ligi hiyo, wachezaji wake wamepoteza hali ya kujiamini na kuruhusu wapinzani wao kutawala michezo.

Kocha huyo alisema kwa sababu hiyo wachezaji wanajiweka katika wakati mgumu kwenye kutumia mbinu ambazo anazifundisha na hivyo amewataka kubadilika mapema.

"Hatujapata matokeo mazuri katika mechi tatu ambazo tumecheza, hivyo inabidi tujikaze ili michezo iliyobakia tupate alama tatu na hatimaye kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi," alisema Lato.

Aliongeza hivi sasa ni kipindi ambacho viongozi wa timu wanatakiwa kuongeza ushirikiano na wachezaji ili kuhakikisha kikosi hicho kinaimarika na kupambana kwa ajili ya kujiepusha na janga la kushuka daraja.

"Mara nyingi timu inapofanya vibaya migogoro huwa ndio inachomoza, mimi naomba katika timu hii hicho kisitokee maana itakuwa ni kuwavuruga zaidi wachezaji, watazidi kupotea na kujiweka kwenye hatari," Lato alisema ambaye timu yake ilichapwa bao 1-0 na vinara wa ligi hiyo KMKM.

# Michezo

Jumapili Machi 14, 2021

Nipashe




## Aguero akanusha kujiunga na Barca

HABARI UK 22

# Yanga: Tutawaliza mapema 2020/21

**Na Adam Fungamwango**

TUTAKOMAA! Hayo ni maneno kutoka kwa Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, baada ya kukubali kuiongoza timu hiyo ambayo ni vinara katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu 2020/21.

Akizungumza na gazeti hili, Mwambusi alisema hakuna kazi nyepesi hivyo yuko tayari kuwaandaa wachezaji wake kupambana kwa ajili ya kusaka matokeo mazuri katika kila mchezo.

Mwambusi, kocha wa zamani wa Mbeya City, alisema katika dunia ya sasa yenye ushindani, hakuna kazi nyepesi, hivyo kila mmoja anatakiwa kupambana kufikia malengo yanayotarajiwa na wadau wanaomzunguka.

"Nina jukumu gumu na siku zote hakuna kazi nyepesi. Hata ukiambiwa kulala tu, kama umeambiwa hiyo ndiyo kazi yako, itakuwa ngumu tu. Na mwalimu siku zote huwezi kusema una kazi ngumu au useme eti huwezi, ni kupambana. Tutapambana, tutahakikisha tunafanya kila njia ili kufikia malengo," Mwambusi alisema.

Kocha huyo aliongeza anawafahamu wachezaji waliopo Yanga, hivyo kazi yake ni kuendeleza pale alipopaacha kwa juhudi za pamoja, timu hiyo itabeba taji la ubingwa wa Ligi Kuu Bara ambalo ndio lengo kuu.

Aliongeza amewakuta wachezaji wana ari, lakini kikosi hakijakamilika kwa sababu baadhi yao wamekwenda kuzitumikia timu zao za taifa na anatarajia watakaporejea, nguvu itaongezeka kwenye timu hiyo.

Kuhusu madai ya kutofautiana na aliyekuwa Kocha Mkuu, Cedric Kaze, alisema hakuwahi kuwa na ugomvi na kocha huyo au yoyote yule katika maisha yake ya kufundisha soka.

Mwambusi alisema aliamua kupumzika kwa ajili ya kupata matibabu kama alivyoshauriwa na daktari wake na si kugombana na Kaze.

"Hakuna kitu kama hicho. Kila mtu anajua mimi niliondoka kwa ajili ya kwenda kupata matibabu. Tuliheshimu uamuzi wa madaktari, lakini kwa sasa wamesema naweza kuendelea, baada ya kwenda tena kufanya vipimo," aliongeza kocha huyo.



Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa na mechi za kufuzu fainali za Afrika dhidi ya Equatorial Guinea na Libya. Kikosi hicho kiliondoka nchini jana mchana na kuelekea Kenya kucheza michezo miwili ya kirafiki na wenyeji wao. **PICHA: MTANDAO**

# MASHABIKI SIMBA WAPIGWA 'STOP'

## ●●●Ni katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Merreikh utakaochezwa...

**Na Saada Akida**

MECHI ya marudiano ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya wenyeji Simba na Al Merreikh kutoka Sudan itakayofanyika keshokutwa Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, itachezwa bila mashabiki, imeelezwa.

Uamuzi huo umefanywa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ambao ndio wasimamizi wa mchezo huo.

Hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa wawakilishi hao wa Tanzania kucheza kwenye uwanja wa nyumbani bila mashabiki wake ambao kwa kiasi kikubwa walikuwa wakiwaongezea hamasa ya kupambana.

Akizungumza jijini jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema klabu yake imepokea taarifa hiyo kupitia kwa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) iliyoeleza CAF imefanya uamuzi huo na unapaswa kutekelezwa.

Manara alisema sababu ya CAF kuzuia mashabiki kuingia uwanjani kushuhudia mechi hiyo ni kutaka kuchukua tahadhari kikamilifu dhidi mlipuko ugonjwa wa COVID 19.

"Katika mkutano mgumu katika maisha yangu ndani ya Simba ni huu, kuwaambia mashabiki wa klabu hii watusamehe kwa uamuzi uliofikiwa na CAF, kucheza bila mashabiki, tunawaomba radhi mashabiki wetu, si matakwa ya Simba, bali ni maelekezo ya CAF na hatuna budi kukubaliana na hilo," alisema Manara.

Hata hivyo kiongozi huyo alisema Simba inaendelea kufanya juhudi mbalimbali kuhakikisha mechi nyingine itakayofuata kuruhusiwa mashabiki kuingia uwanjani.

Alisema baada ya kupokea taarifa hiyo, uongozi unatengeneza taratibu za kuandaa eneo ambalo mashabiki wa Simba watakusanyika kwa pamoja kutoka sehemu mbalimbali ili kuangalia mechi hiyo na kusapoti timu wakati inacheza.

"Tunaomba mashabiki wetu watuombee dua, tushinde mechi ya Jumanne, ngumu sana kucheza bila ya mashabiki, wachezaji watapambana kuhakikisha tunaibuka na ushindi katika mchezo huo, napenda kuwahakikisha kwamba Al Merreikh hatoki kwa Mkapa siku ya Jumanne," alisema Manara.

Alitaja kauli mbiu ya mchezo huo ni 'Silent Killer', wakimaanisha Simba inauma kimya kimya na hivyo ndivyo watakavyofanya siku ya mechi hiyo.

Manara alisema msimu huu wamedhamiria kufanya 'jambo lao' na ni kupambana na hatimaye kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano hayo kwa kuondoka na ushindi dhidi ya Waarabu hao wa Sudan.

"Tukishinda mechi hii basi kutinga robo fainali itakuwa ni jambo rahisi kwetu, kwa sababu mechi ya mwisho tunahitaji pointi mmoja tu, hiyo tunaweza kutafuta katika mechi zetu mbili zitakazobakia dhidi ya AS Vita ya DR Congo tutakayocheza nyumbani au Al Ahly ya Misri huko kwao," Manara alisema.

Msafara wa Al Merreikh uliwasili nchini jana mchana wakati waamuzi ambao wanatoka Afrika Kusini wanatarajiwa kutua jijini kesho Jumatatu.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042